# *Matukio Ya Sasa Yanadhihirishwa Na Unabii*

Na tuinamishe vichwa vyetu. Baba mpenzi wa Mbinguni, tunakushukuru usiku wa leo kwa sababu kwamba Wewe hutujibu maombi. Maskini mwanamke huyu mpendwa anayelala pale, ambapo upasuaji umeshindwa. Lakini, Ee Mungu, tunakumbuka upasuaji wa kwanza uliopata kufanywa duniani, Wewe uliufanya Mwenyewe. Ulitoa ubavuni mwa Adamu, ubavu, ukafunga mkato huo, kisha ukaumba mke. Ee Baba, ninaomba usiku wa leo ya kwamba mkono Wako utashuka sasa na kufanya jambo hili kuu tunaloliomba. Na hawa wengine, Bwana, mwanamke huyu anayeugua ugonjwa wa akili, wengine wote ambao wana maombi, tunawakabidhi tu Kwako, Baba, kwa moyo wetu wote. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Kweli ni majaliwa kuwa hapa usiku wa leo na kuwaangalia wasikilizaji hawa wazuri. Na uimbaji mzuri, kwaya hii ndogo nzuri sana. Nilikuwa tu nikifikiria tofauti, nikiwaona hao wavulana wamesimama pale wakiwa . . . jamaa safi, wamekata nywele vizuri. Nilikuwa nikiwazia, jana usiku, juu ya—juu ya mahali ambapo ninakaa; kundi la majambazi lilishuka likaja pale chini na kujaribu kumzamisha mvulana mmoja kwenye dimbwi la kuogelea; iliwabidi kuita kitu fulani na kuwaondoa pale. Ni tofauti ya jinsi gani, kuona vijana wakisimama, wakiimba nyimbo za Injili; ni tofauti ya jinsi gani.

2 Nikiwazia, kama vile Ndugu Henry alivyosema pale, "hao wanaume wenye hizo nywele ziwapasao wanawake kuwa nazo," unaona. Hiyo—hiyo—hiyo ni kweli. Wanaonekana kama ninii . . . Ninawaona wavulana hawa wakijaribu jambo hilo, kuwa na nywele hizo, hata wanaweka rola za kukunja mle, kuuzunguka uso wao. Nami sijui, mimi . . . wakati mwingine ninavunjwa moyo. Inaonekana kana kwamba ni—ni wakati halisi wa upotovu. Wanaume wanajaribu kuvaa nguo za wanawake, na wanawake wanavaa nguo za wanaume. Na wanaume wakiachilia nywele zao kama wanawake, na wanawake wakiwa na nywele kama za wanaume. Kuna shida gani na watu hawa, hata hivyo? Hivi ninii, kweli, maana hasa ya uadilifu na heshima zimeondoka kwenye taifa hili na kwa watu hawa, ulimwenguni humu?

3 Huu ni wakati mbaya sana, bali ndio wakati wenye utukufu sana ulimwenguni, wa kuhubiri Injili. Kama ningalisimama kwenye ukingo wa wakati kabla haujaanza, na Baba angaliniangalia, na kusema, "Ni wakati gani katika nyakati

hizi zijazo ungetaka kuhubiri?" Ningetaka wakati wa sasa hivi, hiyo ni kweli, kabla tu ya Kuja Kwake.

4 Nikiangalia huko kwa wasikilizaji, walioketi hapa mbele zetu...Rafiki yangu mmoja mhudumu, huko Tucson jana, alikuwa akipanda farasi. (Nikiwazia juu ya mtu huyu mwenye hii...mwanamke huyu mwenye lile gegedu mgongoni mwake.) Farasi huyu alimtupa. Mtu mwingine aliniita saa saba jana usiku, hotelini mwangu, na kusema, "Mtu huyo yuko kwenye Hospitali ya Mashujaa, na macho yake yana mng'ao mbaya, mgongo wake umepondwa, mafigo yake yametokeza, na moyo wake uko karibu kukoma kupiga." Na hapo nikapiga magoti sakafuni, magotini mwangu; simu, nikampata upande huo mwingine, na kumwombea. Naye ndiye huyu hapa ameketi hapa usiku wa leo, ameketi moja kwa moja pale. Hiyo ilikuwa ni jana usiku. Bob, ungeweza tu kusimama hapo? Huyo hapo mtu huyo, yule pale [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Mungu hujibu maombi, asubuhi, usiku, adhuhuri, usiku wa manane, ama wakati wowote.

5 Sasa, mimi—mimi ni mhubiri mwenye maneno mengi sana, kama wanavyosema. Kwa namna fulani ninajisikia vibaya kuanza wakati huu wa usiku, na—nami nilidhani ningekuja tu huku. Hivi majuzi usiku, mbona, tulikuwa tukizungumza huku mahali fulani, na ninii...dakika kumi na tano baada ya mimi kuanza, watu walikuwa wakiokota vyombo, na kuniashiria, "Ondoka! Nyamaza, unapaswa kutoka humu," wakivuta sigara, na kupiga kelele. Haikuwa la—lawama kwa ile dhifa, ni hao watu tuliokodisha kwao. Ndi—ndipo mke wa mwenyekiti akazunguka akaenda akamwambia meneja, kasema...

6 Kasema, "Vema, mnapaswa kutoka humu saa 9:30."

7 Kasema, "Hukuweka hilo kwenye mkataba."

8 Mama huyu, usiku wa leo, alishuka akaja huku (mama mzuri sana) naye akasema, "Tulifahamu ya kwamba mnautaka," kasema, "uchukueni tu kwa muda mrefu mtakavyo." Kwa hiyo hilo...Kwa hiyo ninashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo. Hilo ni jambo zuri sana.

9 Ndugu Henry, hakika ninathamini ukarimu wa—wako wa kunikaribisha hapa, na tawi hili.

10 Nilikuwa na majaliwa jana usiku ya kuwa huku chini kwa Waassemblies of God ambako ninaamini Ndugu Boone ndiye mchungaji. Nilikuwa na wakati mzuri sana kule chini pamoja na kundi hilo la watu. Na kesho usiku tunaenda mahali fulani hapa, sijui ni wapi, na ni tawi lingine. Wanashughulikia hayo; ninaendelea tu kuomba, kusoma, na kuendelea, na ndiyo tu ninayoweza kustahimili.

11 Lakini, sasa, tunaona mambo ya kigeni leo hii. Sasa nimekumbuka mara ya mwisho nilipokuwa hapa ilikuwa katika mkutano wa hema. Ninakumbuka nikizungumzia jambo hilo

jana usiku, juu ya maskini mume na mke waliomleta mtoto wao mchanga aliyekufa. Ni—ni huku juu mahali fulani hapa, waliendesha gari siku nzima na usiku kucha. Maskini mama huyo akiketi, mwenye huzuni, akimshika maskini mtoto huyo mchanga mikononi mwake. Sasa, huenda ameketi papa hapa sasa hivi, nijuavyo mimi. Naye...maskini mume huyo, wakiwa na waume na wake kadhaa, nao walikuwa...Naye akasema... akaniuliza kama ningeweza kuja (huyo mtu aliniuliza) kwenye gari. Nilimtoa mtoto huyo mchanga nje na nilikuwa tu nimemshika; maskini umbo dogo, lililokufa, lililokauka, baridi; ndipo nikaanza kuomba. Na nilipoomba, mwili huo ulianza kusikika kana kwamba unapata joto. Kwa hiyo nikaninii tu...Niliendelea kuomba. Akaanza kurusharusha mateke na kusogea, akiendelea, kwa hiyo mimi...akaanza kulia. Nikamrudishia huyo mama, akarudi naye nyumbani. Kwa hiyo, huenda hata hawakuwa Wakristo, nijuavyo mimi. Unaona? Hilo lilikuwa ni jambo la ajabu.

12 Lakini ninachowazia, usiku wa leo, ninajua kanisa ambalo linakufa, pia, ni watu wetu wa Kipentekoste. Inatubidi kujitikisa tutoke kwenye hali hii, a-ha, hivyo tu. Na jinsi tu tutakavyofanya jambo hilo ni maombi na kujiweka sawa na Neno la Mungu. Ndivyo tu tutakavyofanya jambo hilo. Kuna njia moja tu ya kuepukia, Yeye ndiye njia hiyo, Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Je! tungetaka kanisa letu liingie katika hali kama aliyosema pale, kama vile ilivyo kule Uingereza? Hiyo ndiyo sababu nimekuwa, mnafikiri, mkali sana, nikiwakemea. Wala simaanishi kufanya jambo hilo, ila sitaki kuliona kanisa likiingia katika hali kama hiyo. Hamtaki kuwa katika hali hiyo. Ina—inakubidi tu kulishindilia ndani kwa nguvu sana mpaka ulipigilie na kulishikiza kabisa. Halina budi kutendwa.

13 Kwa hiyo sasa, usiku wa leo, nina ninii tu...Maandiko fulani na kifungu hapa ninachotaka kuzungumzia kwa muda kidogo. Sitasema wakati wowote maalum. Ukichoka, mbona... Huenda nikamalizia katika dakika thelathini, na inategemea tu...Kwa namna fulani daima mimi huliachia tu Roho Mtakatifu, jinsi tu atakavyoongoza.

14 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja tu zaidi, tuzungumze na Mwandishi kabla hatujafungua Kitabu Chake.

15 Mwenyezi Mungu, Mwandishi wa Kitabu hiki, tunaomba kwa Yesu Kristo. Tunashukuru kwa yale tumekwisha kusikia usiku wa leo. Kama tu—tukiitikia mkutano huu kwa kusema, "Amina," na twende nyumbani, ilikuwa ni vema kuwa hapa, kwa kuwa tunajua ya kwamba umekuwa pamoja nasi. Na, Baba, tunapolifungua Neno hili sasa, nena nasi moja kwa moja kutoka kwenye Neno hili, ili tupate kujua saa tunayoishi. Kama tukijua saa tunayoishi, basi tunaweza kujiandaa kwa ajili ya saa hiyo; lakini kama tukiingia vivi hivi bila kujua ni *nini* ama ni *wapi*, basi hatujui jinsi ya kujiandaa. Kwa hiyo, Baba, tunaomba

ya kwamba utatujalia kuona ile Safina pale, na ule Mlango, ukifunguliwa, na Ujumbe ukituita tuingie. Tujalie katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

16 Katika Maandiko Matakatifu, ninataka kusoma fungu hapa; linalopatikana katika Kitabu cha Luka Mtakatifu, kwenye mlango wa 24, ninii. . .Nitaanzia kwenye kifungu cha 13, na kusoma sehemu Yake.

> *Na tazama, siku ile ile watu wawili miongoni mwao walikuwa wakienda* kutoka kwenye *kijiji kimoja, jina lake Emau, kilichokuwa mbali na Yerusalemu kama mwendo wa saa*—saa mbili.
>
> *Nao walikuwa wakizungumza wao kwa wao. . . mambo hayo yote yaliyotukia.*
>
> *Ikawa katika kuzungumza na kuulizana. . .Yesu mwenyewe alikaribia, akaandamana nao.*
>
> *Macho yao yakafumbwa wasimtambue.*
>
> *Akawaambia, Ni maneno gani haya* mnayoongea *hivi* mnapotembea*, na kukunja nyuso zenu?*
>
> *Akajibu mmoja wao, jina lake Kleopa,* akajibu *akamwambia, Je! Wewe peke yako u mgeni katika Yerusalemu, hata* hujayajua mambo haya yote ambayo yametukia. . .*siku hizi?*
>
> *Akawauliza, Mambo gani? Wakamwambia, Mambo ya Yesu wa Nazareti, aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wote,*
>
> *Tena jinsi wakuu wa makuhani na wakubwa wetu walivyomtia katika. . .hukumu ya kufa, wakamsulubisha.*
>
> *Nasi tulikuwa tukitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli.* Mbali na *hayo yote, leo ni siku ya tatu tangu yalipotendeka mambo hayo.*
>
> *Tena, wanawake kadha wa kadha wa kwetu walitushitusha, waliokwenda. . .kaburini*
>
> *. . .Wasiuone mwili wake; wakaja wakasema ya kwamba wametokewa na malaika* waliowaambia. . . *waliosema kwamba yu hai.*
>
> *Na wengine waliokuwa pamoja nasi walikwenda kaburini, wakaona vivyo hivyo kama wale wanawake walivyosema, ila* yeye *wao. . .ila yeye hawakumwona.*
>
> *Akawaambia, Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini (*kutokuamini) *yote waliyosema manabii!*
>
> *Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na* akaingia *katika utukufu wake?*

> *Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza...maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.*

Mungu na aongeze baraka Zake kwa kusomwa kwa Maneno Yake.

17 Sasa nachukua...kama nikiliita somo, ningetaka kuchukua hili: Matukio...*Matukio Ya Sasa Yanadhihirishwa Na Unabii*. Sasa, daima imekuwa ni ninii ya Mungu...njia ya Mungu isiyobadilika kuta-...kuwafanya watu Wake wajue awali kabla matukio fulani hayajatukia.

18 Kama watu katika siku za Bwana Yesu wangalimtafuta tu Mungu na kujua yale yaliyokuwa tu karibu kutimia, wasingemhukumu Yesu kifo. Lakini sababu ya hayo kufanyika, ni kwamba Maandiko yalipaswa kutimizwa, kwa sababu ilibidi Wayahudi wapofushwe. Sote tunajua hilo.

19 Je! mnatambua ya kwamba hilo limeahidiwa tena katika wakati uu huu tunaoishi? Wakati wa Kanisa la Laodikia, wakati huu wa saba wa kanisa tulio ndani yake sasa, ni uchi, wenye mashaka, ni mpofu, wala haujui. Jinsi vile vile alivyowapofusha kule nyuma kwa ajili ya kuupeleka Ujumbe Wake kwa watu walioteuliwa, ameahidi kufanya jambo lilo hilo leo.

20 Na kama ningesema jambo hilo kwa heshima, na kwa ndugu zangu wote na dada katika Kristo, moja ya siku hizi mtu fulani atasema, "Hivi haijaandikwa ya kwamba mambo haya yanapaswa kutukia kwanza?"

21 Na itakuwa vile vile jinsi ilivyokuwa wakati huo, "Amini, nawaambia, amekuja tayari, nao wakamtendea yale waliyotaka."

22 Wakati walipomwuliza, kasema, "Kwa nini, waandishi wanasema, na Maandiko yanasema ya kwamba—ya kwamba 'Imempasa Eliya kuja kwanza.'" Walimwambia Yesu hivyo.

23 Akasema, "Amekwisha kuja tayari, wala hamkumjua." Unaona? Na labda hivyo ndivyo itakavyoishia tena.

24 Sasa tunataka kufahamishwa, kujua yale yatakayotukia kwa kizazi hiki tunachoishi. Mungu amegawa Neno Lake katika kila wakati, kiasi fulani kwa kila wakati, nasi hatuna budi kuona kwamba wakati mmoja hauwezi kuendelea ukaingia katika mwingine. Haiwezekani. Kwa mfano, kama nilivyokwisha kusema, ninaamini jana usiku ama...Ninahubiri daima, usiku baada ya usiku, mahali pengi, na mara nyingine ninatoa tamshi kwa mara ya pili. Sikusudii kurudiarudia maneno yangu. Lakini ninasema hivi: Ingeninii...ingemfaa nini Musa kujaribu kuhubiri ujumbe wa Nuhu? Ama ingefaa nini...ingemfaa nini Yesu kujaribu kuhubiri ujumbe wa Musa? Ama ingemfaa nini Martin Luther kuendelea na ujumbe wa Katoliki? Ingemfaa nini Wesley kuendelea na ujumbe wa Kilutheri? Ingewafaa

nini Wapentekoste kuendelea na ujumbe wa Kimethodisti? Ama itafaa nini Pentekoste kuendelea wakati Bibi-arusi anaitwa? Unaona, tumeingia moja kwa moja katika wakati wa mbegu, tupo hapa katika wakati wa mwisho. Sasa, punje ya ngano isipoanguka ardhini, inabaki peke yake.

25 Kama mkosoaji, kama nilivyokwisha kutoa matamshi tangu kile kitabu kilipotoka, labda mnacho hapa jijini mwe—mwenu, yule mwandishi wa Kijerumani aliyeandika moja ya makala ya kukosoa sana. Yeye ni kafiri. Hakika si . . . Simhukumu kwa sababu yeye amenihukumu sana; lakini, kwa sababu, akiwa ni kafiri, kitabu hicho hakipaswi kuwa kwenye rafu. Basi alisema, "Mungu ambaye angeweza kuketi na kusema angeweza kufungua Bahari ya Shamu na kuwakomboa watu Wake, kisha aketi amekunja mikono Yake tumboni Mwake na kuwaona hao Wakristo katika zile Nyakati za Giza wakiraruliwa vipande-vipande na simba; hao akina mama wenye nywele zilizoloweshwa kwa lami, na kuning'inizwa misalabani na kuchomwa moto; na mtoto wao mchanga . . . mama wajawazito, wangewapasua tumbo lao na kubahatisha kujua jinsia ya mtoto; naye akaketi na kuachilia hayo yatukie; watu waliodhaniwa kwamba ni watumishi wa Mungu huyu."

26 Unaona, Maandiko ni uvuvio. Kamwe hutaweza kuyajua Maandiko kwa kuketi tu chini na kuyasoma kwa msimamo wa kitheolojia, kwa msimamo wa kielimu; kamwe halijafaa kitu.

27 Nilikuwa nikizungumza na mhudumu wa Kibaptisti si muda mrefu uliopita, akasema, "Mpaka tutakapojifunza Kiyunani sanifu, mpaka tutakaponinii . . . "

28 Nikasema, "Katika Baraza la Nikea, kabla ya hapo, walikuwa wakibishania maneno ya Kiyunani katika Biblia." Kamwe hamtaifahamu.

29 Biblia inapaswa kufunuliwa kwa uvuvio. Hicho ndicho kitu cha pekee, ufunuo. Yesu alimwambia Petro, "Juu ya mwamba huu." Mwamba huu wa ufunuo hufunua kwamba Yeye ni nani. "Heri wewe Simoni, mwana wa Yona, mwili na damu havijakufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili; juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu." Si juu ya Petro, si juu ya nafsi Yake, bali juu ya ufunuo wa kiroho ya kwamba Yeye ni nani.

30 Naye ni Neno! Yohana Mt. 1, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu." Waebrania 13:8, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

31 Kwa hiyo tunaishi katika siku ambapo dhihirisho la Neno la Mungu halina budi kuja kwenye wakati tofauti na wakati wa Kipentekoste. Na hiyo ni kweli. Kumbukeni, mtaninii . . . Mimi ni mtu asiye na elimu; lakini mtu huwezi kuyashinda maumbile, kwa kuwa Mungu hutenda kazi katika mwendeleo wa moja kwa

moja pamoja na maumbile. Ni kama tu, kama vile nimekwisha kusema, jua huchomoza na kutua; na linapitia mchana, na kama vile wakati wa shule; nalo linakufa jioni, lipate kufufuka kesho yake asubuhi. Miti huteremsha utomvu wakati wa majira ya baridi kali, unaingia mashinani, kisha unarudi kwenye majira ya kuchipua.

32 Angalieni, Yeye alimlinganisha na punje ya ngano, Bibi-arusi, sababu ya Mungu kuachilia jambo hilo liendelee jinsi hiyo. Hilo Kanisa zuri, halisi, la kweli lililoanzishwa kwenye Siku ya Pentekoste, lilikuwa limekua na kukua tangu Siku ya Pentekoste, likawa kanisa kubwa, ilibidi lianguke ardhini katika ule Wakati wa Giza na kuzikwa kama vile mbegu zote zinavyozikwa. Ilibidi life kusudi lipate kuchipuka katika yale matengenezo tena. Lilichipuka katika yule mtu wa yale matengenezo, Martin Luther. Na kutoka hapo, kama vile tu shina la ngano linavyotokea. Kitu cha kwanza kinachotokea, kuna majani mawili madogo, ndipo linaendelea kuongeza majani zaidi. Moja kwa moja akatokea Martin Luther, na halafu Zwingli, na kuendelea moja kwa moja, Calvin, na walivyoendelea.

33 Hatimaye inaingia kwenye shada. Sasa, huyo alikuwa ni John Wesley katika wakati wa Wesley. Ilikuwa na chavua iliyotokea.

34 Kutoka hapo ukaja wakati wa Kipentekoste, uliofanana sana, kama tu punje halisi ya ngano kama ukiangalia kwenye shina. Lakini kama utachukua hiyo ngano na kuifungua, hakuna hata punje moja ndani yake hata kidogo, ni kapi tu katika *umbo* la punje. Lakini limewekwa pale kwa kusudi fulani, kuikinga punje mpaka . . . Kama jua likiipiga namna *hiyo*, lingeiua.

35 Haina budi kukaa mle ndani mpaka wakati fulani, na Uhai wote unaliacha kapi (kama vile ulivyoliacha shina, ulivyoiacha chavua), unaliacha kapi na kuingia kwenye ngano, na kufanyiza tena kama tu ilivyokuwa kule chini ardhini.

36 Sasa, sote tunajua ya kwamba wakati wowote ujumbe unapotolewa, katika miaka mitatu wanaunda dhehebu. Wanapofanya hivyo, linauua papo hapo; ilifanya hivyo katika siku za Luther, hakika ilifanya hivyo katika siku za Wesley, ilifanya hivyo katika siku za Alexander Campbell, na hao wengine wote, na ilifanya hivyo katika siku za Pentekoste. Hakika! Unaona? Unafikia mahali, kila mmoja anakuwa mgumu, kisha anaenda kombo, nao hawawezi kupokea ufunuo mpya. Wemetulia; nao hao hapo, na hapo wanakufa. Nao Uhai unapitia moja kwa moja humo, na unaenda moja kwa moja kufanyiza ngano. Ndipo ngano inapokuja, Uhai huo ambao umepitia kwenye ngano hiyo, ule ufufuo, unatoa kitu hicho chote nje; naam, unakileta kwa ajili ya Unyakuo.

37 Sasa, kumbukeni, Ujumbe huu ulianza kwanza na uponyaji wa Kiungu, kufanya miujiza. Sasa, kama Mungu akijalia huo upitie kwenye kanisa la kawaida, kama tu vile tulivyokuwa nalo tayari, basi haikuwa ni Mungu. Haimbidi Mungu kujivuna; Yeye haninii—haimbidi kufanya mambo haya, kututumbuiza, kama sisi Wamarekani tulivyozoea kuninii (burudani), bali Yeye hufanya hivyo apate kuvutia usikivu wa watu, ya kwamba Yeye anajiandaa kufanya jambo fulani.

38 Mwangalie Yeye Mwenyewe hapo alipokuja. "Maskini nabii wa ajabu, mwalimu, nabii wa Galilaya." Mbona, huduma Yake ilikuwa nzuri sana, alikaribishwa katika kila kanisa.

39 Lakini siku moja aliketi chini, akasema, "Mimi na Baba Yangu tu Mmoja."

40 "Loo, jamani!" Hilo halikukubalika. "Hatumtaki mtu kama huyo!"

41 "Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, hamna Uhai ndani yenu."

42 "Mbona, yeye ni kifyonza damu! Achaneni na mtu kama huyo!" Unaona?

43 "Unaona, kulikuwa na kitu fulani kilichopaswa kuifuata ishara hiyo. Unaona, kitu fulani kilifuata.

44 Kapi liliishikilia, lakini sasa hilo kapi linaondoka; halina budi kuondoka. Na kumbukeni, miaka ishirini imepita wala hakuna dhehebu lolote lililotoka kwake, wala halitatoka. Tuko katika mwisho wa madhehebu, ngano imepata umbo. Lakini kuna shida gani na ngano sasa, huwezi...haina budi kukaa Uweponi mwa Mwana, ipate kuiva, kabla kivuna hakijaiokota.

45 Sasa, matukio tunayoona yakitukia, yameonyeshwa yakini katika Biblia, kwa kila kizazi. Tunafikiri sote tumeacha njia, bali sivyo, kila kitu kinaambatana tu kabisa na Neno la Mungu.

46 Sasa, Biblia ni kitabu tofauti na kitabu kingine chochote kitakatifu. Hakuna kitabu kama Biblia, kwa sababu Biblia ni Mungu katika umbile la neno. Unaona? Ni...Neno ni wazo lililotamkwa. Mawazo ya Mungu yalilitamka, Maneno Yake kupitia kwa manabii; nao wakaiandika Biblia, ambayo iko katika umbo la neno. Naye Yesu aliliita, "Mbegu." Na mbegu yoyote itazaa kwa jinsi yake kama iko katika hali nzuri, mazingira mazuri. Sasa, Kitabu hiki cha...ni ninii...Kitabu hiki cha unabii, Ki—Kinatabiri juu ya matukio ya usoni. Sasa, Kitabu hiki kina ufunuo kamili wa Yesu Kristo. Huongezi Kwake wala kutoa Kwake, na kila ufunuo hauna budi kuja kupitia Kwake. Unaona, hauna budi kuwa ni Neno.

47 Kwa hiyo watu husema, "Nilikuwa na ufunuo." Ndiyo, tunajua Joseph Smith na wengi walikuwa na mafunuo na kadhalika, bali yalikuwa ni kinyume cha Neno.

48 Hauna budi kuja kulingana na Neno kama unatokana na Mungu, kwa sababu unapaswa kuthibitisha ama kuhakikisha Uwepo wa Mungu. Naye alitangulia kujua mambo haya yote, akiwa. . . Kwa kujua Kwake hapo zamani Yeye alichagua, alitangulia kuchagua (linaitwa katika Biblia "kuchaguliwa tangu zamani") kila wakati mahali pake, na kila mtu mahali pake, na kila mjumbe mahali pake. Yeye ni Mungu, Ibilisi hamdanganyi kwa chochote. Naye ni Mungu, Naye amechagua kila kitu kutukia, na kinaambatana moja kwa moja na Neno Lake.

49 Kwa hiyo kama tunaweza kuona, kwa Neno Lake, ni wakati gani na ni majira gani tunayoishi, mtaliona papa hapa katika Biblia, juu ya wakati huu, kile tunachopaswa. . . kile kinachopaswa kutukia kwenye wakati huu.

50 Sasa, vi—vitabu hivyo vingine, tunaona vitabu vingi sana wanavyoita "vitabu vitakatifu," na kadhalika. Nami nimesoma Ku—Kurani na vingine vingi. Lakini, unaona, vitabu vyao—vyao vitakatifu ni mfumo tu wa maadili, wa uadilifu, ama wa theolojia.

51 Lakini Kitabu hiki ni Nabii, ni tofauti na kitabu kingine chochote. Biblia ni Neno la Mungu linalotabiri mambo ya usoni. Kinatabiri kwa sababu kimeonya awali.

52 Kama Mungu akituma chochote, Yeye anasema na aliahidi katika Biblia ya kwamba asingefanya jambo lolote juu ya nchi mpaka kwanza amelifunulia watumishi Wake manabii. Hiyo ni Amosi 3:7. Yeye. . . wala Mungu hawezi kusema uongo. Yeye hulifunua, hiyo imekuwa ndiyo njia Yake ya kufanya jambo hilo kote katika nyakati. Kamwe Yeye hajawahi kushindwa kufanya jambo hilo.

53 Sasa, tumeahidiwa, katika siku za mwisho, kwamba hili litarejeshwa. Ha—hakutakuwako na kanisa, hakuna dhehebu, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Wapentekoste, kamwe hawataliendeleza (katika hali zao za kisasa) kanisa hili likawa Bibi-arusi. Hawawezi kufanya jambo hilo, wanashindwa. Wanazozana kupita kiasi, na ulimwengu umewanyemelea ukaingia, na kadhalika, na—na wakafa moja kwa moja njiani mwao. Na kwa hiyo Mungu anajua jambo hilo.

54 Na ili kulifunua Neno hili, mtu anasema, "Vema, nina *hili*. Na Mungu abarikiwe, liko namna *hiyo*." Hivyo ndivyo tu ilivyokuwa wakati Yesu alipokuja mara ya kwanza; kila mtu ana fundisho fulani, kila mtu ana *hili*. Itabidi liwe ni jambo fulani lililotumwa kwetu kutoka kwa Mungu. Na Mungu ameliahidi. Na jinsi pekee atakavyofanya jambo hilo, ni—ni kudumisha mtindo Wake ule ule. Aliahidi kututumia, katika siku hizi za mwisho, kulingana na Malaki 4, nabii juu ya nchi, "Ambaye angeigeuza mioyo ya watu, mioyo ya watoto iwarudie baba wa kimitume tena." Aliahidi jambo hilo katika Neno Lake. Luka 17

na mahali pengine pengi ambapo Yeye aliahidi jambo hilo, ya kwamba Yeye. . . yale atakayofanya katika siku hizi za mwisho kuleta kitu hiki kwenye Neno lililothibitishwa.

55 Unaona, mtu anaweza kusema jambo lolote, bali Mungu asipolifasiri Neno hilo. . . Unaona, sasa, tuna fasiri yetu wenyewe, tunasema linamaanisha *hivi*. Na hili, la Kimethodisti, linasema *hivi*, la Kibaptisti linasema *hivi*, la Kipentekoste lilisema *hivi*, la Umoja linasema *hivi*, la Uwili linasema *hivi*. Na, loo, jamani, haya basi. Lakini Mungu hahitaji mfasiri yeyote, Yeye hujifasiria Mwenyewe. Hulifasiri Neno Lake Mwenyewe kwa kulithibitisha katika wakati huo ambao limekusudiwa, wakati ambao limetolewa.

56 Hatuishi katika wakati wa Kipentekoste, tunaishi katika wakati mwingine. Unaona, hatuishi katika wakati wa Kimethodisti, tunaishi katika wakati mwingine. Tunaishi hapa juu kwenye wakati wa Bibi-arusi, kuitwa kwa Kanisa na kulikusanya pamoja kwa ajili ya Kunyakuliwa. Huo ndio wakati tunaoishi. Kwa maoni yangu maaminifu hiyo ni Kweli kabisa.

57 Na Kitabu hiki ni Kitabu cha unabii. Waaminio wake wanaamriwa kukiheshimu na kukisoma, na kumwamini Mwandishi Wake, kwa kuwa kila Neno lililoandikwa humo ndani halina budi kutimia. Kila kitu kilichoahidiwa hakina budi kutimia, kwa kuwa ni Yesu Kristo katika kila wakati. Yeye yule jana, ilikuwa ni Yesu Kristo, aliyekuwa katika Nuhu; ilikuwa ni Yesu Kristo katika Musa, ilikuwa ni Yesu Kristo katika Daudi, ilikuwa ni Yesu Kristo katika Yusufu; ni Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Na ni Yesu Kristo miongoni mwa watu Wake leo, akifanya mambo yale yale aliyoahidi angeyafanya katika wakati huu. Ni Yesu Kristo.

58 Lakini kanisa limekuwa kavu sana, mbali sana, kama vile ndugu alivyosema hapa. Na—na makanisa yetu yanakuwa vivyo hivyo, mpaka hatuna budi kupata kitu cha kututikisa turudi kwenye Neno. Tunajuaje litafanya hivyo? Halina budi kuja kulingana na mpango wa Mungu Mwenyewe. Haliwezi kuletwa na mlei, halitaletwa na mfanyabiashara, haliwezi kuletwa na makanisa. Mungu ameweka mpango Wake.

59 Nilizungumza hapa Shreveport hivi majuzi, katika matangazo ya kitaifa ya redio kote nchini, ya kwamba, *Kujaribu Kumfanyia Mungu Kazi Bila Kuwa Ni Mapenzi Yake*. Daudi alijaribu kulirudisha sanduku la Mungu nyumbani. Yeye alikuwa ni mfalme aliyetiwa mafuta. Mbona, ali—aliwataka shauri wajumbe wa—wake, maakida wake wa maelfu, na makumi elfu, na kadhalika. Nao wote wakasema, “Hilo ni Neno la Bwana.” Nao wakamtaka shauri kuhani, “Hilo lilikuwa ni zuri sana.” Ndipo wote wakavuviwa sana, wakapaza sauti, wakafanya kila tendo la kidini lililokuwapo. Nalo lilikuwa ni

kinyume kabisa cha mapenzi ya Mungu, kwa kuwa kulikuwako na nabii nchini jina lake Nathani wala hata hakutakwa shauri kuhusu jambo hilo. Unaona? Nasi tuliona halikufanikiwa ingawa walikuwa waaminifu, wakijaribu kumtendea Mungu kazi.

60 Nawe unaweza kuwa mwaminifu sana; bali, mpaka tutakapojua tunalofanya, mnapigana na upepo. Rudini kwenye Neno la Mungu na mlainike sawasawa, kisha mwende; ndipo mnajua. Kama vile a—askari, hajui la kufanya mpaka apate amri ya kufanya jambo hilo. Inatupasa kuwa askari wa Kikristo, na kupata amri kutoka kwenye Biblia kwa ajili ya saa hii sasa; si maagizo ya jana, maagizo ya juzi, bali maagizo ya leo hii (njia tutakayopitia). Tupate kujua saa tunayoishi.

61 Matukio haya ya kisasa yanatupita kwa upesi kupita kiasi, na siku moja tutakuta kwamba tutaachwa nyuma bila chochote, na tushikwe, tutiwe muhuri kwa chapa ya mnyama kabla hatujajua.

62 Sasa, na kwa subira inatupasa kungojea jambo hili, kwa kuwa unabii ulioahidiwa, kila mmoja wao hauna budi kutimizwa katika wakati wake. Kwa kuwa unatutabiria, Mwandishi amekwisha kufanya hivi, nasi tunangojea kumwona akilifanya tena. Ni wakati wa jinsi gani tunaoishi! Kitu kama ka—kalenda; unaangalia kalenda upate kujua ni siku gani ya mwaka unayoishi, na unaangalia Biblia ya Mungu kuona ni wakati gani tunaoishi. Hatuishi katika wakati wa Kimethodisti, wakati wa Kibaptisti. Tunaishi katika wakati wa Bibi-arusi, kule kuitwa, kurudishwa kwa Mungu kupitia kwenye mkondo ambao Yeye aliahidi kulirudisha. Aliahidi kufanya jambo hilo.

63 Lakini kama ilivyokuwa katika kila wakati, watu wanamwacha mwanadamu aweke fasiri yake mwenyewe Kwalo kwa theolojia, wala hawataamini thibitisho la Kiungu la Mungu la jambo Hilo (hiyo ni kusema, fasiri ya Mungu); si yale ninayosema, yale mtu mwingine anayosema; bali ni yale Mungu ameahidi na yale Mungu anayofanya, yanathibitisha ya kwamba ni Mungu anayejifasiria Mwenyewe Neno Lake.

64 Waliwaambia ninyi Wapentekoste, miaka arobaini na mitano, hamsini iliyopita. Mama zenu na baba zenu, wakati walipokuwa wapentekoste halisi, walitoka kwenye dhehebu na kukilaani kitu hicho na kutoka kwake. Halafu kama mbwa kwenye matapiko yake, moja kwa moja mkarudi ndani yake tena. Mkafanya jambo lile lile lililoliua kanisa hilo, mlijiua kwa kitu kile kile. Sina kitu dhidi ya watu walio mle ndani, sina kitu dhidi yake, ni mifumo ya kitu hicho ndiyo inayofanya jambo hilo.

65 Nyumbani, mimi. . .kwenda nyumbani. . .Sihubiri jambo hili kwenye mkutano wa mtu mwingine. Nitahubiri *Mburuzo Wa Yule Nyoka*, na muusikilize kama mkizichukua kanda hizo.

66 Na, tazama, walikosa kuona thibitisho la unabii wa Neno la Mungu likitimizwa. Kama makuhani wale. . .Walikuwa wamepanga sawasawa kabisa jinsi Masihi atakavyokuja, walijua kile kitakachotukia. Ma—Mafarisayo walikuwa na wazo lao, Masadukayo, Maherodi, na wengine wote, walikuwa na mawazo yao. Bali Yeye hakuja. . .Alikuja kinyume na kila mmoja wao, bali kulingana na Neno hasa. Yesu alisema jambo lilo hilo lilikuwa lipo hapa: "Kama mngalinijua Mimi, mngaliijua na siku Yangu. Kama mngalijua, mngalininii. . . Mnasema, 'Vema, Musa! Tuna Musa.'" Kasema, "Mbona, kama mngalimwamini Musa, mngaliniamini Mimi; kwa sababu, yeye aliandika habari Zangu."

67 Lakini, unaona, wakati Mungu alipokuwa akithibitisha yale hasa aliyokuwa ameahidi, walikuwa wamejipangia njia fulani ya heshima ambayo Yesu alipaswa kuja, na ninii. . .Ninamaanisha Masihi. Ilibidi Masihi aje moja kwa moja kwenye kundi lao la sivyo hakuwa Masihi. Vema, ndivyo ilivyo, ni karibu hivyo, siku hizi, "Kama huoni kupitia kwenye miwani yangu, huangalii hata kidogo." Unaona, na kwa hiyo hivyo—hivyo ndivyo ili—ilivyo tu. Sisi. . .Hiyo ni kweli. Tunachukia kuwazia jambo hilo, lakini ni Kweli kabisa.

68 Katika Waebrania 1:1, Mungu kwa sehemu nyingi aliandika Biblia kwa njia Yake Mwenyewe aliyoichagua. Hakuiandika kamwe kwa wanatheolojia, wala halifasiri kwa wanatheolojia. Kamwe hapajakuwako na wakati ambapo—ambapo wanatheolojia walipata kuwa na fasiri ya Neno la Mungu. Fasiri huja tu kwa nabii. Na njia pekee tutakayoweza kutoka kwenye mchafuko huu ni Mungu kututumia nabii huyo, kweli kabisa, njia pekee tu litakavyofanywa. Imeaminiwa, imetarajiwa, na—na kutimizwa.

69 Unaona, haikuandikwa na mwanadamu, bali iliandikwa na Mungu. Si kitabu cha mwanadamu, si kitabu cha mwanatheolojia. Ni kitabu cha Mungu, ambacho ni Kitabu cha unabii kilichoandikwa na manabii na kufasiriwa na manabii. Biblia ilisema, "Neno la Bwana linawajia manabii." Hakika!

70 Jinsi hilo lilivyoonyeshwa vizuri, ama, lilidhihirishwa wakati Yesu alipokuja duniani, naye Yohana alikuwa ndiye nabii wa siku ile, na yeye—yeye alikuwa akitabiri. Wao wakasema, "Loo, unataka kusema ya kwamba Mungu atayaangamiza mashirika yetu makubwa hapa na vitu hivi vyote? Na kutakuwako na wakati, wakati hekalu ze—zetu hazitaabudiwa ndani tena?"

71 Akasema, "Wakati ulikuwa unakuja ambapo Mungu angetoa dhabihu ya Mwana-Kondoo wa Mungu, mwanadamu." Naye akasema ya kwamba—ya kwamba yeye angemjua wakati atakapokuja. Kisha akasema. . .Alikuwa na hakika sana na

ujumbe wake, akasema, "Yeye amesimama kati yenu sasa wala hamjui." Yuko mumo humo miongoni mwenu wala hamjui.

72 Ndipo siku moja wakati Yesu alipotoka, Yohana aliangalia juu na akaona ile ishara juu Yake, akasema, "Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Dakika hiyo hiyo Yesu akajua basi ya kwamba amethibitishwa mbele za watu. Sasa, Yeye alikuwa ni Neno, je! tungetilia hilo shaka? Biblia ilisema Yeye alikuwa ni Neno, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa kwetu." Naye ndiye Huyu hapa, nanii. . .Huyu hapa Neno duniani (angalia! kikamilifu!) anatoka moja kwa moja majini anaenda kwa nabii.

73 Hiyo ni kweli, Neno daima humjia nabii Wake. Kwa hiyo hatuwezi kulitarajia kuwajilia wanatheolojia. Hatuwezi kulitarajia kuyajia madhehebu. Halina budi kupitia kwenye njia ya Mungu ambayo alitutabiria, na hivyo ndivyo tu litakavyopata kuja. Litachukiwa, litadharauliwa, litakataliwa. Litakapokuja, litatupwa kando, na kila kitu, bali Mungu atafanya hivyo haidhuru. Lilikataliwa katika Yesu Kristo, lilikataliwa katika Yohana, lilikataliwa na Yeremia, lilikataliwa na Musa. Imekuwa hivyo daima. Lakini Mungu anasonga mbele moja kwa moja jinsi alivyoahidi atafanya. Naam, bwana, Yeye kamwe hakosi kufanya vivyo hivyo.

74 Huyo mtu ambaye ameona ono ama kusikia sauti Yake, kamwe kabisa hakuifahamu. Mara nyingi hakujua, kwa sababu yeye ni chombo tu cha Mungu. Ni mawazo ya Mungu yakitamkwa kupitia kwenye midomo ya mwanadamu; wazo, hasa, ni neno lililotamkwa. Mungu hujichagulia Mwenyewe kwa kuchagua Kwa—Kwake tangu zamani. Yeye alifanya hivyo katika kila wakati, Yeye alimweka mtu kwa ajili ya kila wakati. Kama vile kwa Musa, wakati alipokuwa atimize yale aliyomwambia Ibrahimu. Musa alizaliwa akiwa mtoto mzuri, asingeweza kujizuia kuwa hivyo. Alizaliwa hivyo kwa kuwa alizaliwa kwa ajili ya kusudi hilo.

75 Na kwa hiyo tunaona ya kwamba Mungu hufanya hivyo katika kila wakati. Mungu hujichagulia Mwenyewe kwa kuchagua Kwake alikokusudia tangu zamani, anawachagua manabii Wake na kadhalika kwa ajili ya wakati huo; anaandaa—anaandaa tabia yake, tabia ya mtu huyo, mtindo wa mtu huyo wa kuhubiri, kuhusu karama zao na yote afanyayo, yanakabiliana na changamoto ya siku hiyo. Mungu humuumba mtu huyo na kumtuma. Na katika nia Yake mwenyewe, kama nilivyohubiri jana usiku, sisi ni chembechembe hai ya jeni ya Mungu. Yeye alijua mtu huyo angekuwako katika wakati huo, kabla hakujapata kuwa na molekuli, wala nuru, wala chochote kile duniani.

76 Kwa kuwa wewe ni jeni ya baba yako, nawe ulikuwa katika baba yako, hata hivyo baba yako hakuwa na ushirika pamoja nawe kwa sababu yeye. . .Ulikuwa mle ndani, bali hukujua jambo hilo wala yeye hakulijua, bali ulidhihirishwa upate. . . apate kufanya ushirika pamoja nawe. Nawe kwa kuzaliwa mara ya pili, unazaliwa kwa Uzima wa Milele. Na hiyo ndiyo aina pekee ya Uzima wa Milele, na huo ni Uzima wa Mungu. *Zoe*, neno la Kiyunani ni "*Zoe*," aina moja tu ya Uzima wa Milele.

77 Ndipo endapo wewe ni mwana wa Mungu ama binti ya Mungu, ulikuwa ndani ya Mungu wakati wote. Lakini Yeye alijua utapandwa kwenye tuta gani na katika wakati gani. Kwa hiyo sasa umefanywa kiumbe, mwana wa Mungu, mwana ama binti ya Mungu aliyedhihirishwa upate kukabiliana na changamoto ya wakati huu kumthibitisha Mungu wa kweli na aliye hai wa wakati huu, Ujumbe unaotokea katika wakati huu. Hiyo ni kweli! Ulikuwapo pale kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Kama isingalikuwa. . .Kama hukuwa umechaguliwa namna hiyo, haidhuru utajaribu kiasi gani kuigiza Huo, kamwe hutafanikiwa. Unawezaje kupata damu kutoka kwenye tanipu wakati hakuna damu mle?

78 Hiyo ndiyo sababu ninajaribu kusema kuhusu. . .Watu wakifikiri tulikuwa. . .tunawakemea wanawake kuhusu nywele fupi, na watu wakiniambia kuhusu kusema mambo hayo, "Utaiharibu huduma yako." Ati niharibu huduma ambayo Mungu Mwenyewe aliiweka? Hasha! Na wakati watu wanapolisikia Neno la Mungu. . .Wakati mtoto mchanga anapochukuliwa mimba katika tumbo la uzazi la mama, wakati hiyo seli moja inapoingia mle, seli nyingine huumbika juu ya hiyo. Si seli moja ya mwanadamu, na nyingine ya mbwa, na nyingine ya paka, na hiyo nyingine ya kitu kingine; ni ya binadamu, kabisa, kwelikweli. Na wakati mtu anapozaliwa kwa Roho wa Mungu, yeye haingizi kitu chochote maishani mwake, ni Neno la Mungu lisiloghoshiwa lililothibitishwa kwa wakati huo. Yeye huchukua Neno kamili la Mungu, haongezi kanuni zozote za imani, haongezi kitu kingine chochote ndani Yake. Ni Neno safi la Mungu lisiloghoshiwa, lililodhihirishwa miongoni mwetu.

79 Angalia katika Biblia, unaona ambapo, ni wakati gani tunaoishi basi, wakati unapoona vitu hivi vikuu vikidhihirishwa. Wakati Mungu alipoahidi kufanya jambo hilo, Yeye daima hufanya jambo hilo mwishoni mwa kila wakati kanisa linapofikia mahali pa kugeukia, nalo linageuzwa kutoka kwenye Neno linaingia katika dhambi na anasa. Anasa ni dhambi. Biblia ilisema, "Ukiipenda dunia au mambo ya dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako."

80 Nikizungumza jana usiku, nilikuwa nikizungumza juu ya dha—dhabihu iliyotolewa, Mwana-Kondoo. Ilikuwa iwe ni kwa muda wa siku saba, zikiwakilisha nyakati saba za kanisa.

Hakukupaswa kuweko na chachu yoyote iliyopatikana miongoni mwa watu, hakukuwako na chachu kwa muda wa siku saba. Hiyo inamaanisha ya kwamba hakuna kitu kilichochanganywa Nayo, haijatiwa chachu, kila kipindi. Wala hatutaki kanuni zozote za imani, chachu na kadhalika kuchanganywa nasi. Hatutaki tuchanganywe na ulimwengu. Linapaswa kuwa Mkate wa Mungu usiotiwa chachu, Neno la Mungu, Neno la Mungu lisiloghoshiwa, ambalo, "Mtu ataishi kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

81 Mifumo yetu ya kimadhehebu, na tofauti na kadhalika, imeweka chachu ndani yetu, na *hiki* na *kile* na ulimwengu na mtindo. Na, loo, imefikia mahali ambapo karibu ni Hollywood kila mahali. Hatimaye itakuja mpaka iwe ni kama Uingereza kule, wito wa madhabahuni utaonewa aibu. Jamani! Kama ndugu alivyosema, "Unawezaje kupata samaki katika mtumbwi?" Hiyo ni kweli.

82 Inatubidi kuihubiri Injili katika utimilifu Wake, pamoja na nguvu za Mungu kuthibitisha jambo hilo kulingana na ahadi ya wakati huo na kuthibitisha ya kwamba hayo kabisa ni mapenzi ya Mungu. Nje ya jambo Hilo wewe ni mfuasi tu wa kanisa, haidhuru unajaribu jinsi gani, unajaribu kumfanyia Mungu kazi. Unaweza kwenda kwenye karamu za anasa, huenda ukawa mwaminifu sana kwa kanisa; bali isipokuwa hiyo chembechembe hai ya Uzima wa Milele iwe ilikuwa imechaguliwa awali ndani yako, kuwa mwana ama binti ya Mungu, utakua ukiwa kitu fulani kilichoumbuka; bali kamwe hutakuwa mwana ama binti halisi, wa kweli, wa Mungu.

83 Mara nyingi mimi husimulia hadithi yangu ndogo ya kifaranga cha tai. Jinsi ambavyo mkulima alivyomweka kuku wakati mmoja, naye alikuwa na...Natumaini halisikiki la kukufuru kwenu. Lakini mkulima alimweka kuku, naye alikuwa...alikosa yai moja la kuatamisha. Nina shaka kama mtu yeyote hapa anajua mayai ya kuatamisha ni kitu gani, kwamba huwa na mayai mangapi. Lakini, hata hivyo, yeye alikosa yai moja, hakuwa na ya kutosha. Kwa hiyo akaiba kwenye kiota cha tai, alikuwa na mayai mawili. Naye akaweka hilo yai chini ya kuku.

84 Wakati huyo tai alipoanguliwa miongoni mwa hao kuku wote, alikuwa ndege wa kuchekesha. Asingeweza kufahamu kelele za kuku huyo, hakuzungumza kama nanii wake...kama alivyotaka kumsikia akizungumza. Naye akachakura katika kitalu, na akala toka kwenye kitalu, hakikuwa ni chakula chake. Yeye alikuwa kifaranga cha kuchukiza miongoni mwao. Huyo kuku angelia wala yeye hakuelewa hayo. Kuku angeenda hivi na kula *hiki* na kula *kile*, yeye hakufahamu jambo hilo. Kwa hiyo siku moja nina wake, ama mama, hasa, kwenu. Mimi...huko Kusini tunasema "Nina."

85 Kwa hiyo, haidhuru, yeye. . .mama ya—ya—yake alijua alikuwa na mayai mawili, na ni moja tu kati ya hayo lilikuwa pale, akaenda kulitafuta hilo lingine. Alizunguka kila. . . akavuka nchi, na hatimaye akaruka juu ya kile kitalu. Alimwona kule chini akimfuata maskini yule kuku. Akalia kwa sauti kuu, "Kadogoo! Wewe si kuku, wewe ni tai!" Hilo lilisikika sawa tu kwake. Kwa nini? Yeye kwanza alikuwa ni tai.

86 Na wakati mwanamume ama mwanamke ameketi chini ya kanuni za imani na dini baridi, ya kawaida, kama yeye amechaguliwa kuwa mwana wa Mungu, naye anaona Neno la Mungu likihubiriwa katika nguvu Zake, na Mungu analithibitisha; yeye kwanza ni tai, yeye atalikimbilia kwa hakika tu kama vile mbili mara mbili ni nne. Hawezi kujizuia, kwa sababu tabia yake yenyewe inalipenda Neno la Mungu. Sijali yale mtu mwingine yeyote anayosema, wakati anapoliona Neno la Mungu likidhihirishwa, yeye anaruka kuliendea kwa sababu yeye alikuwa tai mdogo.

87 Wanapoendelea kusema, yeye alisema, "Mama, nitapandaje kutoka hapa?"

88 Naye akasema, "Ruka tu, nitakushika."

89 Hilo ndilo jambo tu unalopaswa kufanya, ni kuruka mara moja usimame kwa miguu yako, mruko mmoja kwa Mungu, ahadi moja, "Bwana Yesu, ninakuamini kwa moyo wangu wote. Ninaamini Ujumbe wa wakati huu. Ninauona ukithibitishwa, na ninajua ni wa kweli." Ruka usimame kwa miguu yako, Mama atakushika. Usijali, wewe ni tai, atakuwa pale moja kwa moja kukuchukua.

90 Sasa, tunatambua ya kwamba tunaishi katika wakati wa kutisha sana na wakati mkuu, lakini wakati kweli za Biblia hii, waaminio wameona hilo limethibitishwa, thibitisho Lake lenyewe hasa ni thibitisho ya kwamba Mungu yumo ndani Yake. Kweli kabisa! Ndipo basi Neno lililoahidiwa, ambalo Mungu aliahidi, linajulikana. Mbegu imepasuka, nao wanaiona na kuiamini. Wengine hawawezi kamwe kuiona, kwa namna fulani wataketi na kuiangalia.

91 Mnajua, nimehubiri kwa nguvu vya kutosha ku—ku. . .kote humu nchini, hivi kwamba hakupaswi kuwako na mwanamke mwenye nywele fupi nchini. Lakini, kila wakati, ninaporudi, kuna wengi zaidi. Kuna shida gani? Kuna kasoro! Mnajua Neno linasema hivyo! Mnasema, "Vema, hilo halileti tofauti yoyote." Linaleta tofauti!

92 Yupo ndugu mmoja mzuri, aliyesema, "Nitakuwekea mikono, Ndugu Branham. Ninakupenda. Unaiharibu huduma yako." Kasema, "Si kazi yako kuwaambia hao wanawake juu ya jambo hilo." Kasema, "Acha wachungaji wawaambie."

93 Nikasema, "Hawawaambii hata hivyo." Nikasema, "Sasa. . . "

94 Akasema, "Vema, si kazi yako, wewe waombee wagonjwa tu."

95 Nikasema, "Ni kazi ya nani, basi? Niliitwa kuihubiri Injili."

96 Kasema, "Nitakuwekea mikono na kumwomba Mungu aiondoe, basi."

97 Nikasema, "Uta—utaniruhusu nikuwekee mikono, pia." Unaona? Nami nikasema, "Nitaomba ya kwamba Mungu atayafungua macho yako nawe utaliona." Kwa hiyo, hiyo ni kweli!

98 Akasema, "Unapaswa kuhubiri . . . Watu wanakuamini wewe kuwa mtumishi, nabii wa Mungu." Akasema, "Unapaswa kuwafundisha hao wanawake jinsi ya ku—ya kupata karama kuu na kutabiri na kadhalika."

99 Nikasema, "Ninawezaje kuwafundisha aljebra wakati hata hawataamini ABC zao, kwanza?" Unaona? Hiyo ni kweli. Kwa hiyo huwezi kufanya jambo hilo. Hilo liko katika kila . . . Hiyo ni kweli. Kama huwezi kufanya mambo ya kawaida, utafanyaje mambo ya kiroho? Mambo ya kawaida. Hakika! Ndugu, dada, huenda likasikika kana kwamba ni mzaha, bali ni Injili! Ni kweli ya Injili. Hiyo ni kweli!

100 Angalia, tunaona leo ya kwamba watu . . . Kuna watu wengi ambao kamwe hawawezi kuliamini, hata watu waliojazwa na Roho. Nitawapa moja ambalo litawakaba koo. Ubatizo wa Roho Mtakatifu haumaanishi ya kwamba wewe utaingia, hata kidogo, si kwa huo, hauna uhusiano wowote na nafsi yako. Huo ni ubatizo, unaona. Hii hapa nafsi ya ndani, *humu* ndani, hiyo inabidi itokane na Mungu. Lakini basi upande wa nje una hisi tano, na tano nje . . . milango ya kuingia kwenye ninii yako . . . kuwasiliana na nyumba yako ya duniani. Upande wa ndani, una roho, na mle ndani una milango mitano: dhamiri yako, na upendo, na kadhalika, milango mitano ya kuingia kwenye hiyo roho. Kumbuka, katika roho hiyo unaweza kubatizwa kwa Roho halisi wa Mungu na hata hivyo upotee. Ni hiyo nafsi iliyo hai, ndiyo iliyochaguliwa na Mungu.

101 Hivi Yesu hakusema, "Wengi watakuja Kwangu siku hiyo, na kusema, 'Bwana, sijatoa pepo, nikafanya kazi kubwa, kubwa mno, nikatabiri, zile karama kuu za Mungu?'" Akasema, "Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu, hata sikuwajua. Wengi watakuja katika siku hiyo."

102 Hivi Kayafa hakutabiri? Yeye alikuwa ibilisi. Tunaona hapo . . . Na hao makuhani, hao watu wakuu, waliodhaniwa kuwa ni watu mashuhuri katika siku hizo, wanyenyekevu na chochote kile, bali wakashindwa kuona Neno la Mungu Lenyewe likidhihirishwa mbele zao.

103 Tungeweza tu kuchukua kundi la hao nilioandika hapa. Vipi kuhusu Balaamu? Yeye alikuwa ninii . . . Unasema, “Mungu hubadilisha nia Yake.” Yeye habadilishi nia Yake!

104 Wakati Balaamu alipotoka akaenda zake kama nabii, naye akaenda kule chini, askofu, mhubiri, vyovyote unavyotaka kumwita, yeye alikuwa ni mtu mashuhuri. Lakini wakati alipomtaka shauri Mungu juu ya kushuka kwenda kule na kuwalaani Israeli; yeye kwanza hakuwapenda. Kwa hiyo alipoomba aende, Mungu alisema, “Usiende!”

105 Ndipo wakamtuma mheshimiwa mmoja, kundi fulani, baadhi yao labda ni maaskofu ama wazee, ama wowote wale, huko chini, elimu zaidi, kumshawishi. Akarudi akamwomba Mungu tena. Haikubidi kumwomba Mungu mara ya pili! Mungu anapolisema kwa mara ya kwanza, hicho Ndicho! Haikubidi kungojea chochote.

106 Rebeka hakungojea kupata ombi lingine. Walimwuliza, kasema, “Je! utaenda?”

107 “Acha aseme.”

108 Akasema, “Nitaenda!” Alikuwa amevuviwa na Mungu kwelikweli. Akawa mmoja wa malkia wa Biblia kwa kutenda kwa mdundo wa Roho wa Mungu aliyetenda kazi juu yake na kupokea kile kilichokuwa ni kweli kabisa, naye akakiamini.

109 Sasa tunaona ya kwamba, Balaamu, bila shaka, hakuweza kuona. Alitoka akaenda na kuwaangalia watu, kasema, “Sasa, hebu kidogo! Sisi ni watu wakuu, mashuhuri sana huku, ninyi ni kundi tu lililotawanyika.” Unaona? “Nasi sote—sote tunamwamini Mungu yule yule.”

110 Hiyo ni kweli. Wote walimwamini Mungu yule yule. Wote wanamwabudu Yehova. Angalia sadaka ya Balaamu: madhabahu saba, namba kamilifu ya Mungu; yale makanisa saba, unaona; kondoo dume saba, zikinena juu ya kuja kwa Bwana. Kimsingi, yeye alikuwa wa kimsingi tu kama Musa alivyokuwa; lakini, unaona, hakukuwa na thibitisho la Kiungu. Kwa hayo, wote wawili walikuwa ni manabii.

111 Lakini chini ya huduma ya Musa, kulikuwa na Nguzo ya Moto ya kimbinguni, Nuru iliyoning’inia kambini. Kulikuwako na uponyaji wa Kiungu, kulikuwako na kelele za Mfalme kambini, ishara kuu, uponyaji wa Kiungu, na maajabu na kadhalika yaliyofanywa miongoni mwao. Ilikuwa ni ishara ya Mungu aliye hai miongoni mwa watu Wake.

112 Kimsingi, wote wawili walikuwa sahihi. Basi Balaamu akajaribu kuwashawishi watu, naye akawaloga akawaingiza katika jambo hilo. Lini? Kabla tu hawajafika kwenye Nchi ya Ahadi. Siku nyingine moja ama mbili, wangekuwa wameingia kwenye Nchi ya Ahadi.

113 Lakini sasa ninahofu . . . Hili ni tamshi gumu kutamka, moja ya siku hizi nitapigwa risasi kwa ajili ya Hilo. Lakini kumbukeni jambo hili, ya kwamba, makanisa yanalogwa na Halmashauri hii ya Ekumeni, anawaingiza moja kwa moja ndani yake, kusema "Ninyi ni kundi moja." Ninyi si kundi moja! Tokeni kwenye upuuzi huo mkatengwe nao! Ndivyo hakika, ni kweli. Tunapaswa kukaa mbali na upuuzi huo, mbali kadiri uwezavyo.

114 Balaamu alisema, "Sisi ni . . . hebu na tuwaruhusu watoto wetu waoane kwa sababu, hata hivyo, tunamwamini Mungu yeye yule."

115 "Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipopatana?" Unawezaje kutembea pamoja na Mungu usipokubaliana na Neno Lake? Unawezaje kuongeza kanuni za imani na kadhalika Kwalo, wakati umechaguliwa usifanye hivyo, ama, umeamriwa usifanye hivyo? Huwezi kufanya hivyo. Hakuna njia ya kufanya jambo hilo, ndugu, dada. Huwezi kuchanganya hiyo chachu na yasiyotiwa chachu. Mafuta na maji havitachanganyikana. Giza na Nuru havitachanganyikana. Nuru ina nguvu sana, huzima tu giza.

116 Na kwa hiyo hatuwezi kuzichanganya pamoja. Wala huwezi kuchanganya dhambi na ulimwengu pamoja. Huwezi kuchanganya Kanisa na dhehebu pamoja. Huwezi kuchanganya Kanisa na kanuni ya imani pamoja. Huwezi kuchanganya ulimwengu na Injili pamoja. Havitachanganyikana! "Tokeni kati yao, mkatengwe nao," asema Mungu, "Nitawakaribisha Kwangu. Mtakuwa wana na binti Zangu, nitakuwa Mungu kwenu." Hatuwezi kamwe kufanya jambo hilo mpaka mambo haya yamedhihirishwa, na Neno la Mungu kwa wakati huu limethibitishwa kuwa ni Kweli. Fuateni nyayo.

117 Pentekoste, hiyo ndiyo sababu Luther alipoteza ujumbe wake. Hivyo ndivyo Wesley alivyopoteza ujumbe wake. Unaona, kama kanisa la Wesley lingaliendelea mbele, wengekuwa ni Wapentekoste. Kama Walutheri wangaliendelea mbele, wangalikuwa ni Wamethodisti. Unaona? Sasa kama Wapentekoste wakiendelea mbele, itakuwa ni Bibi-arusi. Kama mkirudi nyuma na kuendelea kurudi ulimwenguni kama mnavyofanya sasa, mtapotea! Itakuwa tu ni kapi, na shina litachomwa moto. Tunajua jambo hilo. Yeye ataikusanya ngano Yake ghalani. Lakini maganda atayachoma kwa moto usiozimika, ingawa lilikuwa ni bebaji. Bila shaka iliubeba. Lakini huo Uhai uliondoka mara tu ulipofanyika jani, uliendelea kufanya kitu kingine mpaka ukafikia kiwango chake kikamilifu.

118 Na vivyo hivyo Kanisa litapitia katika Kuhesabiwa Haki, Kutakaswa, Ubatizo wa Roho Mtakatifu (kurudishwa kwa karama), moja kwa moja lifikie kwenye umbo la sura ya Kristo. Kristo ndiye Bwana Arusi, Kanisa ni Bibi-arusi, na Bibi-arusi

ni sehemu ya Bwana Arusi. Litapaswa kuwa ni Kanisa la Neno, si kanisa la kimadhehebu. Itabidi liwe ni Kanisa la Neno, Neno lililotambulishwa, na kwa Neno la Mungu lililothibitishwa.

119 Balaamu, asingeweza kuona tofauti. Wengi hawawezi.

120 Farao hakuweza kuliona Hilo, ingawa lilithibitishwa papo hapo mbele zake.

121 Dathani hakuweza kuliona. Dathani alitoka akaja pale nje, naye akamwona Musa na akajua. Alitoka akaenda nje kule, akasema, "Unajaribu kuwazia wewe ndiwe uliye peke yako kwenye kundi lile. Kusanyiko lote ni takatifu!" Mungu kamwe hajawahi kushughulika jinsi hiyo. Alipaswa kuwa amejua vyema kuliko hivyo. Naye akasema, "Vema, kusanyiko lote ni takatifu. Unajaribu kujifanya . . . " Kama tungalilisema siku hizi, maneno ya mtaani, "Changarawe pekee ufukoni."

122 Naye Musa alijua ya kwamba Mungu alikuwa amemtuma huko chini kwa ajili ya jambo hilo. Yeye alisema tu, "Bwana . . . " akaanguka m—mlangoni mwa lile hema.

123 Ndipo Mungu akasema, "Jitengeni naye." Naye akawameza.

124 Basi kumbukeni, ile dhambi ambayo Israeli ilifanya (kwa Balaamu kusema, "Wote tu kitu kimoja."), dhambi hiyo kamwe haikusamehewa Israeli. Hebu angalieni, hebu niwape hesabu ya kushangaza; kutoka katika milioni mbili walioondoka Misri, wawili wao waliingia kwenye Nchi ya Ahadi. Kila mmoja wao alikula kitu kile kile, wote walicheza katika Roho, wote walikuwa na kila kitu shirika; bali ilipofikia wakati wa utengano, Neno lilitenganisha. Ndivyo ilivyo siku hizi! Neno lilitenganisha! Wakati ulipowadia, yeye alisema, "Mbona, hapa, tunaninii . . . "

125 Zitafanana sana, angalia, Biblia ilisema, "Katika siku za mwisho roho hizo mbili," Mathayo 24:24, "zingefanana sana, ingewapoteza walio Wateule kama yamkini." Hilo kapi linafanana kabisa na ngano, bali si ngano. Unaona? Si ngano, lakini linafanana sana nayo. Unaona? Zitafanana sana, ingewapoteza walio Wateule. Mliunda dhehebu na mkaanguka ndani ya dhehebu hilo, na mkakauka na mkafa, nayo ngano ikasonga mbele moja kwa moja kupitia kwa . . . Unaona? Hiyo ni kweli kabisa! Ni bebaji, bali si ngano.

126 Kumbukeni, ngano inasonga tu mbele. Katika ufufuo nguvu hizo zote za ngano zitapanda moja kwa moja ziingie kwenye hiyo ngano, inapoenda kufanyiza kichwa, ipate kutokea katika ule ufufuo mkuu.

Kamwe haikusamehewa!

127 Hebu na tusimame hapa kidogo tu. Ninatumaini siwakabi roho. Lakini, angalieni, hebu niwaulize jambo fulani. Hebu na tuchukue tu hilo. Tuseme, kwa mfano, hesabu hii ingekuwa ni sahihi. Wakati mbegu kutoka kwa dume na kwa jike

inapokuja, kama uliwahi kujua tesitubu ama—ama kuzalishwa na kadhalika kwa ng'ombe, utakuta kwamba ule mshuko kutoka kwa dume hutoa karibu mbegu milioni moja. Na mshuko kutoka kwa jike hutoa mayai milioni moja. Lakini ulijua kuna moja tu kati yao ambalo limerutubishwa? Hao ndama wadogo, ama chochote walicho, katika mamilioni haya ya seli zazi hizi hai, seli zazi hai milioni moja, kutakuwa na maskini seli zazi ndogo moja hai itakayojitokeza miongoni mwa hizo seli zazi hai zingine na kwenda moja kwa moja kule na kulipata hilo yai lililorutubishwa na kujipenyeza ndani yake, halafu hizo zingine zinakufa. Moja ya hizo imechaguliwa kupata uhai, hizi zingine hazijachaguliwa, ingawa zote zinafanana. Moja kutoka katika milioni moja!

128 Vipi kama ingalikuwa hivyo usiku wa leo? Kuna Wakristo milioni mia tano, inavyodhaniwa, nafikiri, Wakristo ulimwenguni, karibu idadi hiyo, hesabu ya kukadiria tu. Kama Unyakuo ungekuja usiku wa leo basi, katika walio hai watakaoondoka, kungekuwa tu na watu mia tano. Vema, kuna kiasi hicho kinachokosekana kila siku, karibu kiasi hicho, ambao hawajui waliko. Bibi-arusi atachukuliwa nasi tutashangaa yote hayo yanahusu nini; na watu wakiendelea moja kwa moja kuhubiri, wakisema "wanapata *hiki*, na *kile*, na *kinginecho*," na hebu angalia ingekuwa ni udanganyifu wa namna gani. Tuseme kama ingekuwa hivyo; sisemi ndivyo ilivyo, sijui mimi, mimi si bingwa wa jambo hilo. Mungu ndiye Hakimu wa hilo. Lakini angalia jinsi lingalitendeka kwa urahisi, katika mifano yote na kadhalika, jinsi lingeweza kuthibitishwa.

129 Kwa nini Kora hakuona jambo Hilo? Kwa nini Dathan hakuona Hilo?

130 Kwa nini Ahabu hakuona jambo Hilo? Wakati Ahabu... Wakati Yehoshafati aliposhuka akaenda kwa Ahabu, alisema, "Ahabu, tuko kwenye shida. Je! Unajua Mungu alitupa nchi hii, Yoshua aliigawanya? Unajua kipande hiki cha ardhi hapa juu ambacho Waashuri wamekichukua, hicho si ni nchi yetu?"

"Naam!"

131 "Watoto wetu wana njaa, na Waashuri (adui wetu) wanawalisha watoto wao, wakijaza matumbo yao kwa ngano inayopaswa kuwa yetu." Hilo ni kweli kimaandiko. Kasema, "Je! Utanisaidia kupanda kwenda kule na kuiteka hiyo?"

132 Sasa, wakati mwingine mtu mzuri chini ya ushawishi wa uovu atakubali kushindwa. Heri mwe waangalifu, enyi kanisa, angalieni kwa makini sana.

133 Sasa, muda si muda mnajua, Yehoshafati, akiwa mtu mashuhuri wa dini, alisema, "Vema, inatupasa kupanda kwenda, hakika, kanisani kwetu, sisi sote ni mtu mmoja." Bali hawakuwa ni kitu kimoja! La! Yeye alisema, "Vema, kanisa letu ni kanisa

lenu, watu wetu ni watu wenu. Hakika, tutaenda," akasema, "bali hebu na tumtake Bwana shauri kwanza."

134 Kwa hiyo akasema, Ee Ahabu, "Hapana shaka, ilitubidi kuwazia juu ya jambo hilo. Vema, tutaninii . . . "

135 "Je! kuna nabii wa Bwana?"

136 Kasema, "Nina seminari nzima iliyojaa ya hao. Nina mia nne hapa chini, walio bora sana. Wote wana Ph.D., L.L.D., zao, L.D. maradufu zao, na chochote kile kinachoambatana nazo. Kila mmoja wao . . . " Sasa kumbukeni, walikuwa ni manabii wa *Kiebrania*, kutoka katika shule ya manabii.

137 Kasema, "Walete, hebu tuwasikie."

138 Sasa, ninaamini ilikuwa ni Zedekia (yule kiongozi mkuu wa askofu, wote) aliyekuja pale, naye alikuwa na uvuvio. Alikuwa na uvuvio, kweli kabisa. Alikuja kule, na akajifanyia pembe mbili kubwa za chuma. Akasema, "Mnajua, BWANA ASEMA HIVI, 'Utachukua pembe hizi na kuwasukuma Waashuri watoke nchini.'"

139 Vema, hao wengine wote walitabiri, "Hiyo ni kweli kabisa!" Kila mmoja wao, seminari nzima, ilipatana. Unaona?

140 Ahabu akasema, "Unaona?"

141 Yehoshafati, kwa namna fulani akiwa ni wa kiroho, mnajua, hakuwa amekauka kabisa, akasema, "Lakini je! hakuna tu mwingine kabisa mahali fulani, ambaye tungeweza kumtaka shauri?"

142 "Unataka kuwataka wengine shauri kwa nini, wakati Ekumeni yote (halmashauri yote), inasema 'Ni sawa'?" (Samahani, unaona.) "Kitu hicho chote kilisema, 'Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya.'" Unaona? "Inatupasa kufanya hivyo."

143 Akasema, "Lakini hivi hakuna mwingine mahali fulani?" Yule wa kipekee, mwajua.

144 Akasema, "Naam, yupo. Yupo mmoja, Mikaya mwana wa Imla, bali ninamchukia." Ndivyo ilivyo daima. "Ninamchukia kwa sababu yeye daima anawakemea watu wetu, na kunilaani mimi, na kuniambia maovu yote juu yangu. Ninamchukia mtu huyo!"

145 Kasema, "Aha, usiache mfalme aseme hivyo." Kasema, "Nenda kamlete."

146 Kwa hiyo wakaenda kule kwa mwana wa Imla, baadhi ya hao—hao maaskofu, ama, baadhi ya wazee, nao wakaenda kule, kasema, "Sasa, hebu sikiliza, je! unataka kurudi kwenye dhehebu tena? Wewe sema neno lile lile wanalosema, watakurudisha."

147 Lakini ilitokea ya kwamba Mungu alikuwa na mtu ambaye wasingeweza kuweka mikono yao juu yake; Mungu alikuwa ameweka mikono yake juu Zake. Yeye alikuwa mwakisi tu wa

Kweli ya Mungu. Kasema, “Hakika,” kasema, “nitashuka niende kule chini, bali nitasema tu yale Mungu atakayoweka kinywani mwangu.” Huyo hapo mtu wa Mungu. Akasema, “Nipeni usiku huu.” Kwa hiyo usiku ukaja, naye Bwana akasema na nabii huyo, maskini mtu asiye chochote. Na muda si muda, akajitokeza kesho yake asubuhi.

Kasema, “Vipi kuhusu jambo hilo, Imla?”

148 Akasema, “Kwea,” kasema, “bali niliona Israeli wametawanyika kama kondoo kilimani, wasio na mchungaji.”

149 Akasema, “Nilikwambia nini! Nilikwambia nini juu ya jambo hilo!” Naye akasema . . .

150 Ndipo yule askofu mkubwa akaenda na kumpiga kofi mdomoni, kasema, “Roho wa Mungu alipitia njia gani? Kwa kuwa ninajua nilikuwa na Roho; nilicheza katika Huyo, nilifanya mambo yote haya. Unaona, ni—nilikuwa na Roho juu yangu. Alipitia wapi?”

151 Sasa, unaona, Imla akiwa ni mwana wa Mungu, ama nabii halisi wa Mungu, alilichunguza ono lake kwa Neno. Kama halikuafikiana na Neno, ni kosa. Unaona? Neno la wakati huo, unaona. Sasa, yeye alisema kimaandiko, nchi hiyo ilikuwa ni mali yao, nchi hiyo ilikuwa ni yao. Kimaandiko, kila kitu kilionekana sawa ila kitu kimoja.

152 Kumbukeni, Neno moja ndilo lililosababisha mchafuko huu wote kutokea, Hawa alikosa kuamini Neno moja la Mungu; mwanzoni mwa Biblia, Neno moja lilisababisha shida. Yesu, akaja katikati ya Biblia, akasema, “Mtu ataishi kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” Mwishoni mwa Biblia, alisema, “Mtu atakayeondoa Neno moja au kuongeza neno moja Kwake.”

153 Si sehemu ya Injili . . . Wamethodisti wana sehemu yake, Wabaptisti, Wapresbiteri, na kadhalika, walikuwa na sehemu Yake, Kotoliki ilikuwa na sehemu Yake, Shahidi wa Yehova, wengine wote.

154 Lakini ni Neno lote, Neno lote, Neno la wakati huu; ndilo muhimu. Wala kamwe hatutafanya hivyo mpaka Mungu atakapomtia mafuta nabii anayeweza kusimama na kulisema, na kulithibitisha, na kulihakikisha ya kwamba ni kweli. Litapenya moja kwa moja kupitia kwa watu, hawatalijua kamwe, kama tu vile imekuwa daima.

155 Ninyi Katoliki, kama vile Joan wa Arc, mlimfunga kwenye nguzo mkamchoma moto kwamba yeye ni mchawi; baadaye mkaifukua miili ya makasisi hao, miaka mia mbili baadaye, na kuitupa mtoni. Hamkumjua Mtakatifu Patrick na wengine wao.

156 Litapitia moja kwa moja mikononi mwenu tena, mnajua muda si muda. Mungu atafanya jambo hilo, wala hata hamtajua limefanywa. Unaona, Yeye anaingia kisiri tu moja kwa moja na

kumchukua Bibi-arusi Wake na kumtwaa moja kwa moja juu, na kumwiba, moja kwa moja miongoni mwa watu.

157 Tunaona basi, maskini huyu Mikaya alisema alichunguza, alijua ya kwamba Mungu alikuwa amesema, kupitia kwa nabii halisi aliyemtangulia. Nabii aliyemtangulia, alisema nini? Alisema hivi, alisema, "Ahabu, kwa kuwa ulimwaga ya mwenye haki, ama damu ya Nabothi mwenye haki, mbwa watairamba damu yako pia, na ya Yezebeli." Na hivyo ndivyo hasa, lilibidi litimie kwa maana Mungu alikuwa amelisema. Nabii huyo angewezaje kutabiri mema wakati maovu yalikuwa dhidi yake?

158 Ninawezaje kuuambia Wakati huu wa Kanisa la Laodikia mambo mazuri wakati Mungu alinena dhidi yake? Ninyi ni uchi, wenye mashaka! Mnasema, "Mimi ni tajiri, nina ninii bora zaidi . . . Nina makanisa kama Methodisti, na Wabaptisti, na Wapresbiteri. Nina *hili*, nina *lile; hiki*, *kile* na *kinginecho* kilicho bora kabisa." Hiyo ni kweli, bali hujui ya kwamba wewe uko uchi, kipofu, mwenye mashaka, kwa jambo halisi ambalo Mungu anadhihirisha. Litapita moja kwa moja katikati yenu, namna hiyo, likitoka moja kwa moja. Unaona? Aminini, enyi watu, kabla ya kuchelewa sana.

159 Sasa, tunaona ya kwamba alimpiga mdomoni, na kusema, "Roho wa Mungu alipitia njia gani . . . ?"

160 Mikaya akasema, "Nilimwona Mungu ameketi kwenye Kiti cha Enzi. Na nanii wote . . . Aliwaita wajumbe wa Mbinguni, kasema, 'Ni nani tunayeweza kumfanya ashuke aende na akamdanganye Ahabu?'" Kasema, "Na roho mmoja wa uongo akapanda akaja na kuanguka mbele za Mungu; mwongo." Basi kumbukeni, huyo roho wa uongo aliwaingia wale manabii, iliwapasa kujua basi kwamba roho aliyekuwa juu yao hakuwa ni kulingana na Neno. Lakini walikuwa wameshawishika sana kwa maana walikuwa ni manabii wa mfalme, kwa kuwa kila kitu kilikuwa shwari kwao.

161 Na hivyo ndivyo kanisa limefanya siku hizi. Mmeondoka kwenye ibada za mtindo wa kale mlizokuwa nazo miaka kadhaa iliyopita wakati mliposimama pembeni mwa barabara na kuihubiri Injili. Mlitoka kwenye madhehebu hayo na kujiita "watu huru!" Hasha! kwa kuwa mmejifunganisha kwake tena, kama nguruwe kwenye kugaagaa kwake ama mbwa kwenye matapiko yake. Kama lilimfanya kutapika mara ya kwanza, litamfanya kutapika tena. Hiyo ni kweli! Mungu aliwatapika kutoka kinywani Mwake, Yeye alisema, "Ninyi ni vuguvugu, si moto wala baridi"; mnafanya mikutano michache, kisha mnacheza kidogo, muziki, na kuimba kidogo, wakati, kabisa ni ninii . . . karibu imekuwa ni fedheha kwa Ukristo.

162 Mwanangu aliniita niende huko hivi majuzi kuangalia televisheni, ilikuwa ni mashindano ya kuimba ambapo watu huja. Hilo kundi la maskini akina Ricky lililosimama pale,

likijitikisa-tikisa kama hii roki, na kuimba hizo nyimbo za dini, ni fedheha kwa Yesu Kristo! Hakuna uchaji tena kanisani hata kidogo. Inaonekana kana kwamba yote imekuwa ni roki fulani, na maonyesho ya mtindo wa nguo, badala ya Kanisa la Mungu aliye hai ambamo Yesu Kristo anaweza kujidhihirisha Mwenyewe katika nguvu. Inaonekana kwangu mimi, kuna kasoro mahali fulani. Wanaanguka. Na Biblia ilisema ingekuwa hivyo. Unaona? Angalieni mahali mlipo. Iweni waangalifu, amkeni kabla ya kuchelewa sana.

163 Sasa tunaona, Yeye alisema, "Ni nani tunayeweza kumtuma huko nje na kumdanganya Ahabu, kumfanya aende kule kuyatimiza maneno ya nabii huyo?" Unaona, kama nabii alisema Neno, mbingu na nchi zitapita bali Hilo haliwezi kushindwa. Halina budi kutimia. Kwa hiyo hivyo ndivyo, ilibidi litimie.

164 Akasema, "Mtieni mtu huyu katika gereza la ndani, mkamlishe chakula cha shida na maji ya shida. Nitakaporudi kwa amani, nitamshughulikia."

165 Mikaya alisimama hapo imara, akijua ya kwamba alikuwa na Roho wa Mungu. Unabii wake, maono yake yalikuwa ni sawa. Ujumbe wake ulikuwa ni sawa, maana ulikuwa ni BWANA ASEMA HIVI kutoka kwenye maono, BWANA ASEMA HIVI kutoka kwenye Neno. Ilibidi liwe ni kweli, lilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI. Alisema, "Kama ukirudi kabisa, Mungu kamwe hakusema na mimi." Nanyi mnajua lililotukia, hakika. Unaona, ninyi . . .

166 Fahamu, ndugu. Sikiliza.

167 Hakika, Kayafa, hakuweza kuliona Hilo. Kwa nini hakuangalia chini . . .? Yeye alikuwa a—alikuwa askofu, alikuwa ni papa wa makanisa yote pamoja. Ni kwa nini mtu huyo hakuweza kumwona Yesu amesimama pale? Kwa nini hakuweza kufahamu? Wakati walipokuwa wakiimba Zaburi ya 23, Zaburi ya 22, hasa, kanisani, na, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Naye yule pale amening'inia msalabani. Maandiko yenyewe hasa, Mungu yule yule waliyekuwa wakimwabudu, walikuwa wakimhukumu na kumwua kwamba yeye ni "shupavu wa dini." Hilo hapo.

168 Lingewashtua kama ningewaambia hilo liko tu karibu ya kujirudia tena. Biblia ilisema Yeye alikuwa yuko nje akijaribu kubisha apate kuingia, wala hakuna mtu angemfungulia, "Yeye nimpendaye ninamrudi na kumkemea, ninamkaripia, ninamtikisa, lakini ni kwa sababu ninampenda. Fungua niingie." Naam. Asingeweza . . . " "Kumbukeni, sikutaka kuingia kanisani; ni *yeye*, mtu binafsi." Yeye asingeweza kuingia kanisani, walimfungia nje. Ila tu . . . ndipo, ndilo dhehebu pekee la hayo yote, ni wakati huu wa kanisa, ambapo Yeye alikuwa nje ya kanisa. Ametolewa nje! Amekatazwa! Amekataliwa! Kwa sababu . . . Yeye alidhihirishwa tu kwa muda

mfupi katika makanisa mengine, katika mfano wa kuhesabiwa haki, kadhalika; lakini humu ndani, wakati unaokuja sasa, ndio dhihirisho kamili la kuthibitishwa kwa Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Loo, nitakubali ya kwamba tuna waigizaji wengi, bali chunguza lile la kwanza, la asili.

169 Musa alishuka akaenda na amri za Mungu, kuwakomboa Israeli; na wakati alipofanya hivyo, alifanya miujiza michache. Waigizaji wakamfuata. Kama wangalikuwa wa kwanza, yeye angalikuwa ndiye mwigizaji. Unaona, yeye alikuwa na Neno la Bwana, naye Bwana akathibitisha; yeye alikaa tu kimya.

170 Na, je! mnajua, jambo lilo hilo limeahidiwa katika siku za mwisho? "Kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa, ndivyo watu hawa walioharibikiwa akili zao kuhusu ile Kweli." Na wakati dhehebu linapoweka ninii . . . linapomchukua mtu na kumwingiza moja kwa moja kwenye dhehebu hilo, ilionyesha ya kwamba halikutoka kwa Mungu; kwa sababu, Mungu hufanya mambo hayo kuivuta mioyo ya watu, ndipo Ujumbe unayafuata. Usipoyafuata, basi si Mungu. Si Mungu! Mungu hufanya hivyo daima.

171 Yuda asingeweza kufahamu jambo hilo. Alitembea moja kwa moja pamoja Naye, hakuliona.

172 Lakini mtu halisi, aliyechaguliwa na Mungu, ile jeni halisi, ile seli zazi halisi, nafsi ya Mungu iliyokuwa ndani ya Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu; kumbukeni, ninyi ambao kweli mna Roho wa Mungu ndani yenu usiku wa leo, mlikuwa hapa katika Kristo kwa sababu Yeye alikuwa utimilifu wa Neno. Yeye alikuwa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Je! mnaamini jambo hilo? Angalieni, Yeye alikuwa ndani ya Kristo. Basi kama ulikuwa ndani ya Mungu, jeni, neno, sifa tangu mwanzo, basi ulitembea pamoja Naye hapa duniani, ulinena Naye duniani, uliteswa pamoja Naye duniani, ulikufa pamoja Naye pale Kalvari, nawe ulifufuka pamoja Naye tena; na sasa umeketi katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu, ukishiriki pamoja Naye (Neno) linapoilisha nafsi yako, ya kwamba, "Mtu ataishi kwa kila Neno litokalo."

173 Si neno la Methodisti, neno la Baptisti; kumbukeni, kama kuna chochote kilichosalia kwenye dhabihu, hakina budi kuteketezwa kabla ya asubuhi, maana kesho ni wakati mwingine wa kanisa. Hiyo ni kweli? Kutoka, ni kweli. Dalili, mfano wa Dhabihu.

174 Mlango. Kasema, "Nitafanya mahali pamoja. Msininii . . . Hamtaniabudia katika kila mlango ambao nimewapa; bali kuna Mlango mmoja, na katika Mlango huo nitaliweka Jina Langu." Na mahali ambapo Bwana atakapoliweka Jina Lake, hapo ndipo Mungu atakapoipokea sadaka yako. Tumefanya kila namna ya milango, bali Mungu alifanya Mlango mmoja. Mungu alifanya

Mlango, na Mlango huo ulikuwa . . . Yohana Mtakatifu mlango wa 10, Yesu alisema, "Mimi ndimi Mlango huo."

175 Mungu aliweka Jina Lake katika Yesu. Je! mnaamini jambo hilo? Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Kila mwana huja katika jina la baba yake. Yeye alisema, "Nilikuja katika Jina la Baba Yangu, hamkunipokea." Nilikuja katika jina la baba yangu, wewe unakuja katika jina la baba yako. Yesu alikuja katika Jina la Baba Yake, kwa hiyo Jina la Baba Yake ni Yesu; kweli kabisa, kwa kuwa alikuja katika Jina la Baba Yake.

176 "Wala hamkunipokea. Mwingine atakuja, naye mtampokea." Mtachukua madhehebu yenu na kuendelea nayo. Endeleeni tu, Biblia ilisema, "Waliinuliwa wapate kupatimiza mahali hapa. Vipofu, uchi, wala hawajui." Kanisa, dini, loo, wacha Mungu sana, kama tu vile Kaini alivyokuwa; alitoa dhabihu, akafanya kila kitu kama tu Habili alivyofanya. Lakini kwa ufunuo ilifunuliwa kwake jinsi hiyo sakramenti ilivyokuwa, si matunda ya kondeni na jambo la kufanya kwa mkono wako.

177 Mwaminio anaweza kuona Neno likifanyika mwili; hao wengine hawawezi kuona.

178 Hao Israeli wote, baada ya kumwona Musa akifanya hivyo na kuwaleta moja kwa moja mpaka kwenye lile baraza kuu, ambapo ilikuwa ifanyiwe, kila mmoja wao alisema, "Tutaambatana na Balaamu, kwa kuwa tunadhani Dk. Balaamu yuko sahihi. Yeye ni mwerevu zaidi, ana elimu kubwa zaidi, kila kitu, kwa hiyo tutachukua tu jambo hilo."

179 Na Mungu kamwe hakuwasamehe, aliwaangamiza papo hapo nyikani. Na Yesu alisema, Mwenyewe, "Hawatakuja kamwe, hakuna hata mmoja wao aliyeokolewa." Yesu alisema . . .

180 Wao walisema, "Baba zetu walikula mana jangwani kwa muda wa miaka arobaini."

181 Yeye akasema, "Kila mmoja wao amekufa, wametengwa Milele na Mungu. Kila mmoja wao amekufa." Hakika! Kwa sababu walisikiliza kosa fulani. Wakati Musa, aliyethibitishwa na Mungu, na kiongozi wa kuwaonyesha njia ya kwenda kwenye nchi ya ahadi, nao walikuwa wamekuja umbali huo vema, lakini basi wasingeendelea pamoja naye.

182 Sasa, waaminio wanaweza kuona jambo hilo, bali wasioamini hawawezi kuliona Hilo limethibitishwa.

183 Angalia jinsi Kayafa alivyokuwa mcha Mungu. Waangalie hao makuhani wote jinsi walivyokuwa wacha Mungu. Na Yesu aligeuka, akasema, "Ninyi ni wa baba yenu ibilisi, na kazi zake mtazifanya."

184 Bali kulikuwa na waaminio wachache wameketi pale. Je! unafikiri hao wanafunzi wangalifahamu wakati Yesu aliposema, "Mimi na Baba Yangu tu mmoja"? Wasingaliweza

kulielezea. Wakati aliposema, "Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, kuinywa Damu Yake, hamna Uzima." Je! wangeweza kulielezea? La. Bali waliliamini, kwa kuwa walimwona Mungu akithibitishwa na kufanyika mwili.

185 Yesu alisema, "Kama sizifanyi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini. Bali kama nikizifanya kazi za Baba Yangu, Neno lililobashiriwa kwamba nitalifanya, basi ninyi . . . Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini zile kazi ninazofanya, mpate kuokolewa." Unaona? Yesu alisema, "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu. Wanalijua Neno Langu, wanaliona wakati linathibitishwa kwa ajili ya wakati huo."

186 "Vema, Kayafa alilijua Neno pia!" Bali si Neno la wakati *huo*. Alikuwa na Neno la mambo yale Mafarisayo waliyokuwa wamemsukumia, bali si Neno lililothibitishwa la wakati huo.

187 "Wanaijua Sauti Yangu, wanaijua ishara Yangu, wanajua maajabu Yangu." Vipi sasa, kuninii . . .

188 Loo, hebu turudi kwenye somo letu, kwa maana tutakosa tu mambo mengi ya Andiko hili tusipolirudia, maana sina budi kufunga katika dakika chache zifuatazo haidhuru, kwa maana itakuwa saa nne katika dakika chache. Ninampenda.

189 Marafiki, ninyi watu mlioshuka mkatembea kwenye ile njia kati ya viti na kuweka sadaka hizo pale muda kidogo uliopita; watu ambao wamewalisha watoto wangu, wakawavika nguo; watu ambao mmeweka fedha zenu (mlizopata kwa jasho) katika sahani ya sadaka, mnajua mahali hizo zinakokwenda? Hizo husaidia kunipeleka katika nchi za ng'ambo kwa makafiri ambao kamwe hawajasikia chochote kuhusu Mungu. Hivyo ndivyo ninavyofanya nazo, kila senti, Mungu ndiye hakimu wangu. Hawa hapa baadhi ya nanii wangu . . . mtu huyo anayeketi papa hapa sasa ambaye yuko katika—katika hazina ya kanisa langu. Mimi hupata dola mia moja kwa juma, na ni hizo tu; zilizosalia hutumika katika kudhamini mikutano ya nchi za ng'ambo ambako wao hawawezi kuja.

190 Makanisa hayatanialika. Hawanitaki. La. Hiyo ni kweli! Wananiita sasa, "Yeye ni . . ." Wanasema, "Yeye ni 'Yesu Pekee,' ama yeye ni kitu kama hicho, ama mwasi fulani, mshupavu wa dini, na yote kama hayo, Je—Jezebeli." Nami ni—ninatarajia jambo hilo, walimwita Bwana wangu, "Yezebeli," na wakamwita . . . si Yezebeli, bali "Beelzebuli." Walimwita hayo majina yote mabaya. "Ikiwa walimwita Mwenye nyumba, 'Beelzebuli,' si zaidi wale walio wa wanafunzi Wake?" Kwa hiyo hilo halileti tofauti yoyote.

191 Na wewe mwenyewe, kwa msaada wa Mungu, unafikiri ningesimama hapa, mnafiki mkubwa, na kuwaambia jambo fulani . . .? Ama, si ningejiweka sawa na jambo hilo kama niliwaza lilitoka kwa Mungu?

192 Bali kama ninawapenda na ninajua yaliyo Kweli. . .Je! mmepata kunisikia nikisema jambo lolote katika Jina la Bwana ila lile lililotimia? La. Ninamwuliza mtu yeyote. Kuna maelfu ya mambo ambayo yamesemwa, yote yanatimia. Je! mnakumbuka ule wakati ambapo Samweli aliitwa, ninaamini ilikuwa hivyo, naye akasema. . .? Israeli walitaka kujifanya kama mataifa mengine. Huko ndiko ninyi Wapentekoste mnakoelekea. Mnataka kufanya kama watu wengine. Ninyi si watu wa aina hiyo. Kaeni mbali na jambo hilo. Makanisa makubwa na mambo makubwa mazuri, Ee ndugu, msifanye hivyo. Tunahubiri kuja kwa Bwana kumekaribia, hebu na tuingie kwenye huduma huko kwa makafiri na kuwapasha habari. Unaona, fanya kitu kuhusu jambo hilo.

193 Lakini, unaona, Samweli alisema, "Je! Nimepata wakati fulani kuchukua fedha zozote zenu kutoka kwenu kwa ajili ya riziki yangu?"

194 Wakasema, "La, Samweli, hujapata kufanya jambo hilo."

195 Kasema, "Je! nimepata kuwaambia lolote katika Jina la Bwana ila lile lililotimia?"

196 "Loo, hilo ni kweli, Samweli. Tunaamini wewe ni nabii aliyetumwa kutoka kwa Mungu. Naam, bwana. Kila kitu ulichosema kilitimia, Samweli. Lakini tunataka jambo hilo haidhuru." Unaona lililotukia. Ee ndugu, Maandiko yanaendelea tu kujirudia hapa na pale kote katika Maandiko, maana ndiyo njia ya Mungu ya kufanya jambo hilo, unaona. Unaona, mnafikia nyakati kama hizi.

197 Hebu na tuliendee somo letu upesi sana. Sasa, nimechukua muda huu wote, na hata sijalifikia somo langu bado.

198 Liko moyoni mwangu! Ninawapenda! Msiangamie pamoja na ulimwengu! Kama ninyi ni wa ulimwengu, mtaangamia pamoja na ulimwengu. Kama ninyi ni wa Mungu, mtaenda pamoja Naye katika ufufuo. Kwa hiyo badilisheni tabia zenu usiku wa leo kutoka kwenye kuipenda dunia na mambo yaliyo katika dunia, na kanuni hizi zote za imani na kadhalika, na mwangalie moja kwa moja huko Kalvari kwenye Dhabihu yenu; mkutane Naye huko katika masharti hayo, kwa maana hapo ndipo mahali pekee atakapopata kukutana nanyi. Yeye. . .

199 Wamethodisti wanasema, "Ni katika kanisa letu"; Wabaptisti wanasema, na Wapentekoste, na *hili*, na Wapresbiteri, na *hili*.

200 Lakini Yeye alisema, "Nitakutana nao mahali pamoja, Mahali nilipoweka Jina Langu." Hapo ni katika Yesu Kristo. Hapo ndipo Mungu alipoweka Jina Lake. Hapo ndipo mahali pekee atakapokutana nawe; na hapo ni Kristo, ni Neno, yeye yule jana. . .Limekua kutoka miguuni, mapajani. Na sasa liko kwenye kichwa, likijitayarisha kuondoka; likimdhihirisha Bibi-arusi katika kipimo kikamilifu, kama Bwana arusi.

201 Sasa hebu tuliendee somo letu, upesi sana, kwa kama dakika kumi, na ndipo tutafunga. Sasa somo letu, sote tutataka kulitafakari. Lilikuwa limetukia tena, kama somo letu, kama vile lilivyotukia kwa kawaida.

202 Mungu alimtuma nabii Wake kama vile Yeye. . .Neno lilikuwa limeahidi katika Malaki 3, "Nitampeleka mjumbe mbele ya uso Wangu kutangulia kuja Kwake."

203 Sasa kama unataka kuhakikisha jambo hilo, kulithibitisha; Mathayo, mlango wa 11, inathibitisha jambo lilo hilo. Wakati wanafunzi wa Yohana walipokuja na wakamwona Yesu, wao walisema, "Yohana yumo gerezani." Kasema, "Tumekuja kukuuliza kama yeye. . . "

204 Jicho la Yohana la tai lilikuwa limeingia utando. Naye alikuwa gerezani, alikuwa karibu kufa; kasema, "Nendeni mkamwulize."

205 Unaona, Yohana alisema, "Loo, pepeto Lake li mkononi Mwake, Yeye atausafisha sana uwanda Wake." Alidhani ule Utawala wa Miaka Elfu utaanza papo hapo, alidhani nafaka ilikuwa tayari. Bali ilibidi ife na kuingia kwenye shina, ipande juu tena imfanye Bibi-arusi wa kweli. Kwa hiyo akasema, "Yeye ataikusanya ngano Yake ghalani, na ataiteketeza, kwa moto." Mwangalie yule—yule mtangulizi wa Kristo katika wakati *huo*, kile alichosema kingetukia. "Nafaka. . . "

206 Nami ninatumaini hamjalala. Nafaka iko hapa! Itakusanywa ghalani. Ilikuwa ni Bibi-arusi huyo, sehemu ya hiyo. Lakini Yeye alisema ni nini kitakacholipata shina? Litateketezwa kwa moto usiozimika. Utafute wokovu sasa wakati ukiweza. Kuwa nafaka, sio shina. Unaona? Ingia katika Uzima, sio utaratibu wa kale uliokufa; ingia katika Uhai wa Kristo, Neno lililodhihirishwa, ninii. . .lililodhihirishwa na kuthibitishwa kuwa kweli. Huu ndio—huu ndio wakati wa kukusanya, kivuna kinakuja. Afadhali uingie kwenye nafaka, maana kapi litaachwa nyuma.

207 Sasa, tunakuta kwamba lilitukia, Yesu. . .Kumalizia nukuu yangu hapa, hii Mathayo 11. Unaona, Yeye hakumpa Yohana. . .Alisema, "Sasa, ngojeni, nitampa Yohana kitabu juu ya vile atakavyojiongoza, *Mwaminio Akiwa Gerezani.*" La! Yeye alisema, "Simameni huku mwone kitakachotukia. Rudini mkamwambie Yohana mambo yanayotendeka: viwete wanatembea, vipofu wanapata kuona, wafu wanafufuliwa, na Injili inahubiriwa kwa maskini." Vile vile kabisa nabii alivyosema ingetukia. "Na heri ninyi msiochukizwa Nami."

208 Ndipo wanafunzi Wake wakaanza kukingama kilima, Yeye akageuka, akasema, "Mlitoka kwenda kuona nini mlipoenda kumwona Yohana? Je! mlienda kumwona mtu anayeshughulika na mavazi mororo, na kadhalika, kosi zilizopinduliwa, na haya yote, mwajua?" Kasema, "Wamo katika nyumba za wafalme,

wanawabusu watoto wachanga na kuwazika wafu, hajui jinsi ya kuushika upanga ushikwao kuwili." Unaona? Kasema, "Mlienda kuona nini? U—unyasi unaotikiswa na upepo wowote, 'Njoo huku, Yohana, nitakupa fedha nyingi zaidi kama ukija huku'? ('Vema, Mungu abarikiwe, mimi si Mmethodisti tena, nitakuwa Mpentekoste, nitakuwa Mpresbiteri, nitakuwa wa *hili*, *lile*, lile lililo na fedha nyingi zaidi.')" Kasema, "Kamwe hamkuona unyasi unaotikiswa na upepo." Kasema, "Mlienda kuona nini kule, nabii?" Akasema, "Naam, na zaidi ya nabii."

209 Yohana ndio kwanza ampe Yesu sifa duni sana angaliweza kumpa. Alijua ilibidi itokee namna hiyo; alimwuliza baada ya yeye kumtambulisha na kuona ile Ishara juu Yake, akasema, "Huyu *ndiye* Masihi," kisha anakuja na kuuliza, "Je! Wewe Ndiye, au tumtazamie mwingine?"

210 Lakini, angalia, Yesu akijua hilo, aligeuka na akampa sifa, kasema, "Mlitoka kwenda kuona nini, unyasi ukitikiswa na upepo?" Kasema, "Hapajakuwapo na mtu aliyezaliwa na mwanamke aliye mkuu kama Yohana, hata siku hii." Hiyo ni kweli! Ni sifa ya jinsi gani kumpa mtu huyo!

211 Lakini, unaona, lilikuwa ndilo hilo hapo, unabii ulikuwa umetimizwa moja kwa moja mbele ya uso wao, kwa kuja kwa mtangulizi, vile vile hasa alivyosema Malaki. Sasa, hiyo ni Malaki 3, siyo Malaki 4.

212 Yohana Mbatizaji alikuwa ni Malaki 3, Yesu alisema hivyo. Wakati walipomwuliza, kasema, "Kwa nini waandishi wanasema . . . "

Kasema, "Yeye amekwisha kuja. Walifanya yale waliyosema."

213 Lakini, kumbukeni, Malaki 4, mara baada ya nabii wa Malaki 4, kule kuja kwa nne kwa Yohana Mbatizaji katika . . . ama ninii . . . kwa Eliya. Kule kuja kwa tano kutakuwa Ufunuo 2, wale mashahidi, wakati atakapokuja kwa ajili ya masalio ya Wayahudi. Lakini Mungu ametumia Roho yuyo huyo mara tano: neema, J-e-s-u-s, imekuwa ni Yesu wakati wote; i-m-a-n-i, n-e-e-m-a, na kadhalika. Unaona? Namba tano ni namba ya neema na Yeye aliitumia. Hatatumia tu tatu, hatatumia tu mbili, tatu, nne. Anaitumia mara tano.

214 Sasa, angalia upesi sasa, tunapomalizia. Yeye alisema, "Huyu ndiye aliyenenwa habari zake, 'Ninamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu.'"

215 Lakini katika Malaki 4, mara baada ya nabii *huyo* kutabiri, ulimwengu mzima utachomwa moto, na wenye haki watatembea nje juu ya majivu ya waovu. Unaona? Kweli kabisa! Unaona, huo ni unabii wa Malaki 4.

216 Na tazama katika Luka 17, ambapo Yeye alisema, "Katika siku za mwisho, itakuwa kama Sodoma na Gomora tena."

Je! tumelipata? Tuna Sodoma na Gomora tena? Mataifa yote, angalieni. Angalieni yale yaliyosemwa hivi karibuni kuhusu Uingereza, kitu hicho chote kimepotoka. Hata chakula kimepotoshwa. Na angalieni hapa yale sayansi . . . Mmeona katika *Reader's Digest*, ninaamini ni mwezi uliopita, wao walisema, "Wavulana wadogo na wasichana wanapitia kwenye umri wa makamu kati ya miaka ishirini na ishirini na mitano." Mimi hukutana nao mkutanoni, wasichana wadogo katika kukoma hedhi, na umri wa miaka ishirini, ishirini na miwili, katika kukoma hedhi. Inatokana na nini? Ule upotovu, uchotara. Hicho ndicho kilichopotosha hasa, kitu hicho chote kimeupotosha mwili. Sisi si kitu ila takataka za—za . . . kama tu mmea chotara.

217 Hebu chukua mmea chotara na uuweke pale nje, kila kijidudu kitaukimbilia moja kwa moja. Lakini mmea halisi, wa asili, kijidudu kitaukimbia, hakiwezi kusimama juu yake. Na hiyo ndiyo shida ya kanisa, tumelifanya chotara.

218 Hiyo ndiyo shida ya maskini farasi wa Pearry Green kule juu, naye alimtupa mvulana yule hivi majuzi, yeye si kitu ila maskini robo farasi wa kale. Unaona? Jambo tu ni kwamba, yeye . . . Ni kama nyumbu tu, yeye ni—yeye ni . . . nyumbu hajui baba yake ama mama yake ni nani, hajui chochote; yeye ni nusu nyumbu na nusu farasi, na nusu *huyu* na punda; yeye hajui kwamba ni nani. Usingeweza kamwe . . . Yeye atangojea maishani mwake mwote apate kukupiga teke. Hiyo ni kweli! Unaweza kumwita, useme, "Njoo huku, mvulana. Njoo huku, mvulana." Atayainua masikio yake juu, na, "Hoo! Hoo! Hoo!" Unaona?

219 Kama baadhi ya hawa wanaosema "Siku za miujiza zimepita, Hoo! Hoo! Hoo!" hawa machotara wote, wanaodhaniwa kuwa wafuasi wa kanisa na Wakristo. Sisemi jambo hilo kwa utani, bali ni Kweli. Lakini ndugu, halisi, wa uzao bora, yeye anajua baba yake alikuwa ni nani, mama yake alikuwa ni nani, babu yake alikuwa ni nani, bibi yake alikuwa ni nani, unaweza kumfundisha jambo fulani, yeye ni muungwana.

220 Na Mkristo halisi aliyezaliwa na Roho Mtakatifu na kujazwa na nguvu za Mungu na Neno, yeye anajua baba yake ni nani, mama yake ni nani, babu yake ni nani, bibi yake alikuwa ni nani, anajua yote kuhusu jambo Hilo. Unaweza kumfundisha jambo fulani.

221 Lakini chotara, hayo ndiyo yaliyoyapata makanisa. Chotara kati ya ulimwengu na madhehebu ya dini, na kuweka Neno kidogo ndani yake *hapa*, Neno kidogo *pale*, la kutosha tu kudanganyia. Hiyo ni kweli. Unapoona Neno halisi la Mungu likidhihirishwa kama vile Kayafa na hao wengine walivyofanya, wanaliacha, hawajui. Machotara!

222 Sasa tunaona, na katika ujumbe huu, Isaya 40:3 pia ilimthibitisha Yohana. Yeye alisema, "Sauti ya mtu, nabii, aliaye

nyikani, 'Itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni mapito yake.'" Kanisa halikumwamini, kwa maana hakuwa wa kundi lao. Nabii huyo alilelewa nyikani, akakua pasipo kumjua mtu yeyote. Alikuwa na Roho yule yule juu yake ambaye Eliya alikuwa Naye: alikuwa mtu wa nyikani, aliwachukia wanawake wachafu.

223 Mnakumbuka vile Eliya…Ni kitu gani kilisababisha kichwa chake kuondolewa kwake? Ilikuwa ni Yezebeli. Yezebeli ndiye aliyesababisha kifo chake. Alimfukuza akaenda nyikani.

224 Yohana Mbatizaji, mtu mwingine aliyependa nyika, mwindaji, mtu wa mwituni. Hebu mwangalie. Hakuwa na elimu. Angalia fungu la—lake la maneno, hakuwa kama mwanatheolojia. Alisema, "Enyi wazao wa nyoka!" Kitu kilicho kichafu sana unachoweza kupata nyikani, kule kuvizia, kilikuwa—kilikuwa ni nyoka. Ndipo akawaita hao makuhani, "Enyi wazao wa nyoka! Ni nani aliyewaonya ninyi kuikimbia ghadhabu itakayokuja? Msianze kusema, 'Sisi ni wafuasi wa *hili*, na tuna *hili* ama *lile*,' kwa maana ninawaambia, Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya," nyika. Pia, "Shoka" (kile alichotumia) "limekwisha kuwekwa penye shina la mti; basi kila mti usiozaa tunda zuri, hukatwa na kutupwa motoni." Amina.

225 Yeye alikuwa mhubiri wa maumbile. Mtu mashuhuri wa Mungu, aliishi muda mfupi, bali hakika aliwasha moto kote nchini. Alikistaajabisha kizazi hicho katika miezi sita ya huduma yake. Mungu alimlea kwa muda wa miaka thelathini, kusudi apate miezi hiyo sita kutoka kwake. Lakini Mungu hufanya njia Yake Mwenyewe, anajua kwamba mavuno Yake ni nini.

226 Nasi tunaona sasa ya kwamba hili ndilo hasa lililokuwa limetukia. Hawakumwamini, kwa maana hakuwa wa kundi lao. Hawakumwamini. Walifanya kama kawaida, hawakuliona. Hawakuliamini Neno la Mungu la Malaki 3, vinginevyo wangaliona dhahiri, kwa maandiko, ya kwamba huyu alikuwa ndiye yule mtangulizi. Hawakuwa na nabii kwa muda wa miaka mia nne, na hapa mmoja anajitokeza jukwaani mara moja. Unaona? Na hao watu, hao waaminio, walimwamini kuwa ndiye. Unaona, hawakuamini jambo Hilo. Hawakuamini, kwa maana walipoona maandiko hayo yakithibitishwa kabisa, yale Yeye aliyosema angefanya, na kila kitu, na kuliona limethibitishwa dhahiri wakati Neno lilipoingia moja kwa moja majini likaenda kwa nabii huyo. Hao hapo wamesimama.

227 Kuna wengi wanaobishania Andiko hilo hapo juu ya Yohana. Unaona, Yohana alisema, "Nahitaji kubatizwa na Wewe, Nawe waja kwangu kwa nini?"

228 Yesu akasema, "Kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo…lakini ndivyo itupasavyo, inatupasa (kutupasa) kwamba tutimize haki yote. Yohana, wewe ukiwa nabii, unajua dhabihu haina budi

kuoshwa kabla haijatolewa. Nami Ndiye hiyo Dhabihu, nawe ni nabii na unajua hivyo." Ndipo akamkubali na kumbatiza. Unaona? Naye alijua ndivyo ilivyokuwa.

229 Angalia, walimcheka, wakamwita "mshupavu wa dini, mshenzi, domo kaya, asiye na elimu," kama kawaida, huyo nabii aliyekutangulia kuja kwa mara ya kwanza kwa Yesu.

230 Sisemi ya kwamba wao ni . . . hawana uigaji ule ule leo wa—wa kilicho halisi. Wanao, wanao kabisa. Lakini, kumbukeni, unapoona dola ya bandia hapana budi kuweko na dola ya kweli ambayo imetengenezewa kutokana na hiyo. Mahali unapoona mtu akiigiza kuwa Mkristo, hapana budi kuwako na Mkristo halisi mahali fulani; kwa sababu, kama sivyo, *huyo* angekuwa ndiye wa asili. Huna budi kufikia kwenye kitu cha asili. Lakini chunguza ya kwanza, uone kama ya asili inaambatana vilivyo na ahadi. Kama inaambatana, basi iamini: ahadi ya wakati huo.

231 Ndipo unabii wa Yohana ulithibitishwa katika utaratibu wa Mungu. Neno lilimjia nabii na kumthibitisha kwamba kweli yeye ndiye mtu huyo.

232 Tena Yesu alikuja katika ninii . . . tofauti na walivyoelewa unabii huo. Hawakuuelewa namna hiyo. (Sasa, tunaelekea kumalizia sasa.) Lakini kulingana na Neno la nabii, Huo ulitimizwa kikamilifu. Unabii umetimia; bali jinsi walivyodhani ingekuwa, haikuwa hivyo. Sasa, wangewezaje kuelewa na wajue ni upi ulikuwa wa kweli na ni upi wa uongo? Kuona kama lilikuwa limethibitishwa na Mungu, kama ilikuwa ni Mungu akifasiri yale aliyosema. Kulikuwako na Yesu wengi wa uongo walioinuka, na kumwongoza mtu, kundi la . . . watu mia nne, huko nje jangwani na kadhalika; bali hakuthibitisha kujidhihirisha mwenyewe katika Neno, unaona, kama Yeye alivyosema.

233 Yesu, wakati alipokuja, Yeye alikuwa awe nabii. Hiyo ni kweli! Na leo hii, kabla Yesu hajaja tena, dhihirisho kamili la utu wa Yesu Kristo utadhihirishwa katika mwili. Wazia jambo hilo! Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu, wakati Mwana wa Adamu atakapokuwa akifunuliwa." *Kufunuliwa* ni nini? Kufahamika wazi, kutambulishwa. Siri imekwisha kuletwa, ikafunuliwa. Katika siku atakayofunuliwa Mwana wa Adamu, ulimwengu utakuwa katika hali ya Sodoma. Tunao, sivyo? Naam! Ni wangapi wanaoamini jambo hilo? Uko katika hali ya Sodoma. Na hiyo ni kweli kabisa! Angalia mahali ulipo, sasa.

234 Kumbukeni, daima kuna makundi matatu ya watu katika kila kundi la watu mnalokusanya, hayo ni, wanaojifanya waaminio, wasioamini, na waaminio. Tunao katika kila kikundi. Wamekuwa nao wakati wote. Kulikuwako na Wasodoma,

kulikuwako—kulikuwako na Walutu, na kulikuwako na Ibrahimu.

235 La Ibrahimu lilikuwa ni kundi lililoitwa litoke, hakuwa Sodoma kwanza. Sasa angalieni Ujumbe wao! Walikuwa wakimtazamia mwana aliyeahidiwa, wakamtarajia kwa miaka kadhaa. Mungu alikwisha mwonyesha Ibrahimu ishara nyingi kuu na maajabu, lakini hapa Mungu alishuka Mwenyewe akaja kama mtu!

236 Unasema, "Huyo alikuwa ni Malaika."

237 Ibrahimu alimwita, "Bwana," herufi kubwa za B-w-a-n-a. Msomaji yeyote wa Biblia anajua ya kwamba B-w-a-n-a katika herufi kubwa ni Elohimu. "Hapo mwanzo Mungu," Bwana Mungu, Elohimu, Yeye ajitoshelezaye kwa yote. Ibrahimu alimwita, "Bwana Mungu, Elohimu."

238 Sasa angalia, kulikuwako na watu wawili walioshuka kwenda Sodoma wakiwa na ujumbe, nao wakawahubiria Wasodoma. Hawakufanya chochote, bali waliwapofusha; ambapo, kuhubiri Injili kweli humpofusha asiyeamini.

239 Lakini angalia ni ishara ya namna gani ambayo kundi la Ibrahimu lilipokea!

240 Sasa, sisi tunapaswa kuwa Uzao wa kifalme wa Ibrahimu, Isaka alikuwa ni uzao wa kawaida. Lakini Uzao wa imani, imani katika Neno lililoahidiwa, Neno *lililoahidiwa* (msikose jambo hilo) ulikuwa ni huo Uzao wa kifalme; huo ndio uliokuwa ule Uzao, imani ya Ibrahimu. "Sisi tukiisha kufa katika Kristo, sisi ni Uzao wa Ibrahimu, warithi pamoja naye kulingana na ahadi."

241 Angalia wakati hayo yote yalipokuwa yakitukia, huko chini Sodoma kulikuwa na wahudumu wawili huko chini wakihubiri wakiwa na ujumbe mkuu.

242 Kulikuwa na mmoja aliyeketi hapa pamoja na kundi la Ibrahimu ambaye hakujipumbaza na kundi lile kule chini. Sasa angalia yule aliyekaa pamoja na kundi la Ibrahimu, kwamba aliwapa ishara ya namna gani. Yeye alisema . . . .Sasa, kumbukeni, jina lake lilikuwa ni Abramu siku chache kabla ya hapo; naye ni S-a-r-a-i, sio S-a-r-a (binti mfalme). Naye Mtu huyu, akiwa ameelekeza mgongo Wake hemani . . .

243 Wanawake wakati huo walikuwa tofauti na jinsi walivyo sasa. Inawabidi kutoka nje na kuchukua biashara za bwana zao na chochote kile, mwajua. Lakini hawakufanya hivyo siku hizo; walikaa huko nyuma.

244 Kwa hiyo wao . . . kwa hiyo hao Malaika walioketi pale. Yule Mjumbe, Naye akasema, "Ibrahimu, yu wapi (S-a-r-a) Sara mkeo?" Yeye alijuaje? Alilijuaje hilo?

245 Ibrahimu akasema, "Yuko hemani nyuma Yako."

246 Akasema, “Nitakurudia kulingana na wakati niliokuahidi. Nitakurudia.” Na kwa namna fulani Sara akacheka moyoni.

247 Akiwa ameelekeza mgongo Wake hemani, Naye akasema, “Mbona Sara amecheka, akisema, ‘Mambo haya yanawezekanaje?’” Kama asingalikuwa katika Ibrahimu, bibi-arusi wake wakati huo, Mungu angalimwua. Vivyo hivyo na sisi pia leo pamoja na kutokuamini kwetu kote, kama tusingalikuwa katika Kristo. Hilo linatushikilia papo hapo, unaona. Asingemdhuru wala asingemchukua Sara bila ya kumdhuru Ibrahimu. Unaona?

248 Na kwa hiyo kumbukeni, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Tunaona kila mtu akikubali ya kwamba dunia iko katika hali ya Sodoma. Nilichukua gazeti la Los Angeles hapa si muda mrefu uliopita, nalo likasema, nafikiri ni “Ulawiti unaongezeka asilimia ishirini au thelathini katika Los Angeles, kila mwaka ukiongezeka kiasi hicho.” Ni . . . Loo, ni chukizo! Katika serikali yetu na kila mahali, kila kitu kimekuwa upotovu tu. Hiyo ni kweli! Kitu hicho chote, mfumo huo wote, kanisa na chochote kile vimepotoka. Ni wakati uliopotoka.

249 Sasa nataka kuwauliza ninyi wanatheolojia jambo fulani, linalohusu ndugu zangu. Sineni dhidi yenu, ndugu yangu mpendwa; niko hapa kukusaidia, ndugu. Niko hapa kusimama juu ya yale Neno la Mungu linayosema kuwa ni kweli, kuushika mkono wako na kuutoa umati huu wa watu kwenye upuuzi huu. Kweli!

250 Lakini angalia hapa, hatujapata kuwa na mjumbe huko Sodoma hapo awali ambaye jina lake linaishia na h-a-m mpaka sasa. Tumekuwa na akina Spurgeon, Wesley, Luther, na chochote kile, bali kamwe si mjumbe wa kimataifa ambaye jina lake linaishia kwa h-a-m, huko nyuma. Hiyo ni kweli! Unaona, G-r-a-h-a-m, herufi sita, G-r-a-h-a-m, Billy Graham; yule mwinjilisti mashuhuri, kazi kuu ya Mungu, mtu huyo ametumwa kutoka kwa Mungu. Yeye ana huko kuhesabiwa haki vizuri sana, naye analitikisa taifa kwake, unaona, namna hiyo. Hakuna . . .

251 Mwangalie Oral Roberts kwa dhehebu la Kipentekoste. Ni lini kumepata kuwapo na mmoja kama huyo?

252 Herufi sita, si saba. Ibrahimu ni A-b-r-a-h-a-m, saba. Billy Graham ni G-r-a-h-a-m, sita.

253 Sasa angalia hao wajumbe. Angalia wakati tuliomo, hapajakuwapo na wakati kama huo katika historia. Angalia ishara zile zile alizoahidi zingepewa kila kikundi. Angalia mahali walipo. Pale pale, hasa, mahali penyewe, wamekaa katika utaratibu. Maumbile, ulimwengu, kila kitu, kimekaa sawa kabisa katika majira yake.

254 Sasa usikose jambo Hilo, tunapoyachunguza Maandiko mengine! Upesi sasa, kwa kuwa ninawachelewesha sana. Kuita. . . Angalieni hapa. Na kulingana na nabii, yeye alikuja kwa Neno hasa, kwenye wakati unaofaa hasa.

255 Sasa angalia wakati tunaoishi sasa. Je! hatuishi moja kwa moja katika wakati huo wa Sodoma? Mwangalie yule mjumbe wa kundi la Ibrahimu. Angalia hizo namba, herufi, na hesabu ya jina lake. Unasema, "Jina halina maana yoyote." Kamwe usimwache mtu yeyote akwambie jambo hilo. Kwa nini akabadilisha jina la Abramu, likawa Ibrahimu, Sarai likawa Sara? Kwa nini akabadilisha la Simoni likawa Petro, na hao wengine wote? Unaona? Hakika ipo. Hakika!

256 Hiyo ndiyo sababu ninasema usininii, kamwe usimwite mtoto wako "Ricky," ama "Elvis," ama kitu fulani. *Elvis* maana yake ni "paka," *Ricky* ni "panya." Unaona, unaposema. . . Hiyo ni kweli kabisa. "Les," ama kitu fulani, kamwe usimwite mmoja wa mtoto wako. . . watoto wako hilo. Kama ndivyo, libadilisheni upesi sana, enyi watu. Msininii. . . Ninyi ambao. . . Kama mnaamini mimi ni mtumishi wa Mungu, usilibandike jina hilo kwa maskini mtoto huyo. Unaona? La, bwana, mpe jina lingine mbali na hilo. Jamani! Hainipasi kwenda kando katika jambo hilo, maana nimeliacha somo langu, bali nililisema na liko kila mahali. Mimi. . . Hivyo ndivyo unavyofanya, hujui wakati unapolisema. Unaona?

257 Wakamwita, "Mgeni, mpiga ramli, ibilisi, Beelzebuli," na kusema, "Alijifanya Mwenyewe Mungu." Loo, jamani!

258 Hivi nabii Isaya hakusema, "Ataitwa Mungu mwenye nguvu"? Isaya 9:6, "Kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume, na uweza wa kifalme utakuwa mabegani Mwake, Naye ataitwa Jina Lake Mshauri, Mfalme wa Amani, na Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa milele." Hiyo ni kweli! Pia, Yohana Mt. 1:1, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu." Mnaamini hilo? Yeye hakuwa ninii tu. . . Alikuwa nabii, bali alikuwa zaidi ya nabii; alikuwa Mungu-nabii. Kwa nini ikambidi kuja?

259 Kumbukeni, Yeye anakuja katika majina matatu ya mwana. Alikuja kwanza katika jina la Mwana wa Adamu. Kamwe hakujiita "Mwana wa Mungu." Mnajua hilo. Unaona, Yeye alikuja katika Mwana wa Adamu, nabii. Yehova Mwenyewe, Baba, alimwita Yeremia, "mwana wa Adamu"; nabii ni mwana wa Adamu. Yeye alikuja. . .

260 Sasa Yeye alikuja baada ya Siku ya Pentekoste, alirudi katika mfano wa Roho Mtakatifu, Roho wa kimbinguni. Sasa Yeye ni Mwana wa Mungu.

261 Katika ule Utawala wa Miaka Elfu Yeye atakuwa Mwana wa Daudi, akiketi juu ya kiti cha enzi cha Daudi. Unaona,

Yeye anakuja katika . . . Yeye ni Mwana wa Mungu, Mwana wa Adamu, Mwana wa Daudi.

262 Loo, Biblia imejaa vito hivi. Hatuwezi kuvipata vyote katika usiku mmoja. Lakini inafaa tu kuweka hili sasa. Kesho huenda isipambazuke. Huenda tukawa tumeondoka kabla ya kesho. Huenda nikawa ninamhubiria mtu ambaye huenda akafa kabla ya asubuhi. Ninaweza nikaondoka kabla ya asubuhi. Ndugu, dada, hiyo si hadithi ya kujibunia, hiyo ni kweli halisi! Hatujui tutaondoka wakati gani, wala hutapata nafasi yoyote baada ya hiyo pumzi ya mwisho kuuacha mwili wako. Jiweke sawa sasa hivi, usingoje mpaka asubuhi, huenda ikawa imechelewa sana.

263 Angalia sasa, walikuwa wamemtendea vile vile hasa manabii walivyosema wangefanya, kama tu wanavyofanya hata siku ii hii katika Wakati wa Laodikia. Kama ukitaka kuangalia jambo hilo, soma Ufunuo 3, "Vipofu, uchi, wala hamjui. Kumfukuza Kristo . . . " Wakati anapoanza kujifunua Mwenyewe katika mfano wa mbegu tena, ile ile iliyoingia ardhini ikarudi kuwa Bibi-arusi; Bibi-arusi tu na Bwana arusi, ni mwili ule ule tu na damu ile ile, huduma ile ile, na mambo yale yale, akifanya vile hasa Yeye alivyofanya; yule Roho.

264 Na hawa hapa wakiiga na kufanya chochote kile, na kila mmoja ana kitabu chake na anakimbia, na *hili*. Loo, hujapata kusikia mihemko kama hiyo! Na . . . [Ndugu Branham anavuta pumzi kwa pua yake—Mh.] "Ninasikia harufu ya pepo sasa." Yote *haya*, *yale,* kinyume cha kimaandiko tu iwezavyo kuwa!

265 Na kitu kilicho halisi kikiwa moja kwa moja pale mbele yao, wanaondoka, "Hao si wafuasi wa dhehebu langu." Jamani, jamani, ninii tu, unaona, vipofu tu wakiwaongoza vipofu wenzao. Hivi hawataanguka wote shimoni? Wamepofushwa na mapokeo ya kimadhehebu ya binadamu, wanamtoa kanisani mwao kama vile Mungu alivyosema wangefanya, katika Ufunuo 3; kama kawaida, kama ilivyotabiriwa.

266 Angalia jinsi Yesu alivyoninii . . . .alivyojitambulisha kwa hawa wanafunzi, sasa, nasi tutafunga. Hawa wanafunzi wawili, Kayafa . . . Kileopa, hasa, na rafiki yake. Sasa tuko katika ufufuo, ile asubuhi baada ya ufufuo, ufufuo wa kwanza; ni asubuhi nzuri jinsi gani, Yesu amefufuka kutoka kwa wafu na anaishi miongoni mwa watu Wake. Ni wazo zuri jinsi gani!

267 Yeye yupo hapa leo kama alivyokuwa siku hiyo, kwa sababu ni yeye yule jana, leo, na hata . . . Na kujifunua Mwenyewe zaidi leo kuliko alivyowahi kujifunua katika wakati mwingine wowote tangu siku hiyo; tumepitia kwenye ngano na shina na kapi (vyote vimepita sasa), tumeingia katika ngano tena. Unaona, tumerudi kwenye punje.

268 Kujulikana kama . . . kujua . . . Angalia jinsi alivyojitambulisha Mwenyewe kwa watu hawa, sasa, kumbukeni, kama Masihi wao (kabla tu hatujafunga) wa Neno

lililoahidiwa la wakati huu. Angalieni! Yeye aliwatokea, kwa . . . kama alivyosema angefanya, kwa manabii. Angalia, “Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote manabii wameandika kumhusu Yeye yalibidi kutimia.”

269 Mwangalieni Yeye! Anarejea moja kwa moja kwenye Neno la Mungu, Yeye hakuja moja kwa moja na kuwaambia, “Hivi ninyi hamnijui? Mimi Ndiye Masihi aliyefufuka.” Kamwe hakusema hivyo. Unaona, Yeye aliwapa tu Maandiko; kama vile Yohana alivyofanya, na hao wengine. Unaona? Yeye alininii tu . . . Inawabidi kupata hilo wenyewe. Inawabidi kujiamulia. Sasa, msilale, jiamulieni.

270 “Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote manabii wamesema yalipaswa kutimia.” Ni kemeo la jinsi gani kwa wale waliodai walimjua. Unaona?

271 Angalieni jinsi alivyoliendea jambo hilo. Yeye hakujielezea waziwazi kabisa, kama nilivyosema dakika chache zilizopita, na kusema, “Vema, hivi hamjui Mimi Ndiye Masihi wenu wa wakati huu? Hivi hamjui Mimi Ndiye?” Mtumishi halisi wa Mungu kamwe hajitambulishi jinsi hiyo; Maandiko humtambulisha kwamba Yeye ni nani. Hakika, atafanya hivyo. Lakini aliwakumbusha yale manabii walikuwa wamesema wachunguze katika wakati wa Masihi. Unaona hilo? Turudi nyuma moja kwa moja: “Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito, kutokuamini ya kwamba yote waliyosema manabii kumhusu Masihi yanapaswa kutimia.”

272 Yeye, kama vile Yohana, aliacha Neno la Biblia limtambulishe, kile alichokuwa kwao. Hilo lilipaswa kuwa dhahiri vya kutosha. Kama Neno lilikuwa limemtambulisha, huyo anapaswa kweli kuwa Ndiye ile ahadi waliyokuwa wakiitazamia. Walijua alikuwa . . . ilibidi mtu fulani kutokea jukwaani kwenye wakati huo.

273 Mbona, Yeye alisema, “Sasa hebu niwaonyeshe kile Neno linasema kinapaswa kutukia katika siku hii.”

274 Mimi sio mimi, usiku wa leo, ninayejaribu kuwaambia, Neno kwa Neno (hata mahali penyewe, eneo, majina, namba, chochote kile, na ishara zote, nyakati, na kila kitu), ya kwamba tupo papa hapa kwenye wakati wa mwisho? Hakika mnaweza kuona kile ninachonena habari zake. Unaona? Angalieni! Hilo ni dhahiri sana halihitaji utambulisho zaidi. Yeye alisema, wakati alipokuwa humu duniani, “Yachunguzeni Maandiko, ndani yake mnadhani mna Uzima wa Milele, hayo ndiyo . . . yanashuhudia kile nilicho Mimi, unaona, kwamba Mimi ni nani.”

275 Angalieni, Yeye alianza na nabii Musa, nabii, Kumbukumbu la Torati 18:15. Ninayaangalia Maandiko hapa. Kumbukumbu la Torati 18:15, Musa alisema, “Bwana Mungu wako . . . ”

276 Unaona, Mungu alisema naye juu ya mlima. Na, loo, jamani, zile ngurumo; wao wakasema, "Acha—acha Bwana. . . Acha Musa anene, sio Mungu, tusije tukaangamia."

277 Akasema "Wao walisema vema. Nitaninii. . . Sitasema nao tena namna hii, bali nitawainulia nabii." Na huo ndio umekuwa ujumbe Wake daima. Huo ndio utakaotatua jambo hilo lote hapo mwisho. Hauna budi tu, kwa maana Neno la Bwana halina budi kumjia nabii. Hicho ndicho kitu pekee linachoweza kukijia. Lisipokuja, linavunja Neno la Mungu na kumfanya Yeye aseme jambo lisilo kweli. Unaona? Kamwe halitaenda kwenye seminari. Linamwendea nabii. Naye nabii anatumwa kutoka kwa Mungu, akiwa amechaguliwa. Na jinsi unavyojua amechaguliwa, na si vile mtu huyo alivyosema, . . .

278 Tumekuwa na akina Eliya, na makoti, na chochote kile, na majoho, na kila namna ya upuuzi, na tukaingia katika umadhehebu na chochote kile.

279 Lakini kutakuja humu duniani, kwa ahadi ya Mungu, mtumishi halisi wa Mungu, aliyetambulishwa na Mungu (kwa Neno Lake likiwa ndilo jawabu la siku hii), ambaye atamweka Bibi-arusi katika utaratibu (uchache halisi wa kanisa) na kumnyakua. Hiyo ni kweli! Atamtambulisha, "Tazama, yule pale Yule niliyesema habari Zake, unaona, atakayekuja."

280 Na yote ambayo manabii walikuwa wamesema kumhusu Yeye, na kwa ajili ya wakati huu, mbona hakika ingekuwa ni jambo la kufurahisha kumsikia Yeye akisema hivyo. Hivi usingetaka kumsikia akisema hivyo? "Manabii wote walinena kuhusu. . . " Kumbukeni, Yeye alisema yale manabii wangesema kumhusu Yeye, akijinukuu Mwenyewe, yale aliyokuwa amesema (Naye alikuwa ni Neno); akinukuu.

281 Sasa hebu tusikilize Maneno aliyonukuu. Mngetaka kusikia yale aliyowaambia? Hebu tu tuyaendeleze mazungumzo yao sasa, kabla tu hatujafunga.

282 Sasa, walielezewa juu ya matukio ya karibuni ya kule kusulubishwa, juu ya hadithi ya pale kaburini na jiwe la kaburi, na wale wanawake waliokuwa wamemwona, na mwingine aliyesema wamemwona, na kadhalika. Akasema. . . Wa—walimwelezea hayo kwa kifupi. Naye anaendelea moja kwa moja na Neno kuhusu. . . akijinukuu Mwenyewe katika Neno:

"Sasa angalieni katika Zekaria 12." (Hapana budi alinukuu Zekaria 11:12.) "Kwa maana aliuzwa kwa vipande thelathini vya fedha. Je! Masihi hakupaswa kuuzwa kwa vipande thelathini vya fedha?

"Katika Zaburi 41:9, Yeye alisalitiwa na rafiki Zake. Unaona?

"Zekaria 13:7, aliachwa na wanafunzi Wake.

"Katika Zaburi 35:11, alishtakiwa na mashahidi wa uongo.

"Kwa Isaya 35:7, alinyamaza mbele ya washtaki Wake, hakufunua kinywa Chake." (Vema, bwana.)

"Isaya 50:6, alipigwa mijeledi.

"Zaburi 22—22, Yeye alilia msalabani, 'Mungu Wangu, mbona umeniacha?' Mifupa Yangu yote inanikodolea macho. Walizua mikono Yangu na miguu Yangu." (Angalia unabii ambao Yeye angezungumza habari zake!)

"Isaya 9:6, Kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, bikira atachukua mimba, kadhalika.

"Na pia Zaburi 22:18, wa—wa—waligawanya mavazi Yake miongoni mwao.

"Isaya 7:14, bikira atachukua mimba.

"Zaburi 22:7 na 8, walimfanyia. . .alidhihakiwa na adui Zake, nanii Wake. . .waliodhaniwa kwamba ni marafiki Zake; adui Zake, kanisa.

"Katika Zaburi 22 tena, Yeye alininii. . .hakuna mfupa uliopaswa kuvunjwa, bali walimzua mikono na miguu.

"Isaya 53:12, alikufa pamoja na hao wakosao.

"Katika Isaya 53:9, alijeruhiwa, na kuzikwa pamoja na ndugu tajiri.

"Katika Zaburi 16:10, Yeye alifufuka toka kwa wafu. Daudi alisema hivyo, 'Sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu.' Alifufuka toka kwa wafu.

"Malaki 3, Yohana Mbatizaji alikuwa mtangulizi Wake."

283 Na kila mifano ambayo huenda aliiendea! Hata kwa Isaka akiwa mfano Wake juu ya Mlima. . . juu ya mlima ambapo baba yake Ibrahimu alimpeleka, katika Mwanzo 22.

284 Hapo ndipo walipoanza kuona ni nani alikuwa ametimiza Maandiko yaliyoahidiwa kwa ajili ya siku hiyo. Hapo ndipo, baada ya kuchelewa, walipoanza kuona. "Loo! Vema, ngoja kidogo! Mnajua nini?" Walijua basi ya kwamba Rafiki yao aliyesulubiwa, Yesu, alikuwa ndiye yule Nabii aliyeahidiwa. Walijua kwa sababu . . . Unaona, hawakuwa wameelezewa juu ya Maandiko.

285 "Lakini, hapa, mambo haya yote yanayopaswa kutukia msalabani, mambo haya yote. Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kufahamu yote ambayo wamesema manabii; jinsi ambavyo Masihi atateseka, na kuingia katika utukufu Wake, na kufufuka katika siku ya tatu."

286 Bado wanaendelea. "Na hiyo ni kweli. Ninasema Yeye—Yeye. . .Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu?" walisema. Si ajabu mioyo yao iliwaka! Unabii aliokuwa akitoa ambao ulitimizwa.

287 Ndipo wakaanza kufahamu ya kwamba Rafiki yao, Mtu ambaye walikula pamoja Naye, wakasema Naye, wakashirikiana Naye, wakavua samaki pamoja Naye, wakalala mwituni, kwamba Ndiye alitimiza kila Neno la majira yaliyoahidiwa! Hilo hapo. Walikuwa wametembea maili sita, ilionekana kana kwamba ni muda mfupi sana, nakisia, nao walikuwa wamesikia mahubiri ya saa sita juu ya unabii uliothibitishwa (mrefu kidogo kuliko ule tumekuwa nao usiku wa leo, unaona). Sasa kwa namna fulani wakati wa jioni ulikuwa unapita, Nuru za jioni zilikuwa zimekuja.

288 Ni wakati ule ule sasa, kanisa! Nuru za jioni zimekuja! Waebrania 13:8, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Loo, matukio yakidhihirishwa na unabii, vile vile leo. Nuru ya jioni iliyoahidiwa na nabii wa Mungu, katika Zekaria 14:7, huenda ikafungua tena macho ya mwaminio wa kweli aone matukio yanayotukia leo, ambayo yamethibitishwa na unabii ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho. Yesu anakuja.

289 Ninii hasa . . . Ni . . .

290 Yeye alisema, "Kutakuwako na siku ambayo haitaitwa usiku wala mchana." Alisema, "Lakini wakati wa jioni kutakuwako Nuru." Sasa, tunajua, kijiografia, jua huchomoza mashariki na kutua magharibi. Sasa, nabii alisema, "Kutakuwako na wakati mrefu ambao utakuwa wa utusitusi, kwa namna fulani . . . usingeitwa mchana wala usiku; kwa namna fulani ni siku yenye giza, utusitusi."

291 Sasa, Mwana alichomozea wapi? Je! . . . Huyo alikuwa M-w-a-n-a tunayenena habari Zake sasa. Ya kwamba m-w-a-n-a wa kawaida huchomoza mashariki na kutua magharibi. Mungu yeye yule, hasa . . . *Jua* hasa. Na M-w-a-n-a wa Mungu alichomoza kwanza mashariki, kwa watu wa mashariki.

292 Na sasa baada ya Yeye kuondoka, walifanya nini? Miaka mia tatu baadaye, waliunda dhehebu lao la kwanza, kanisa Katoliki la Kirumi. Wakapitia kwenye ule Wakati wa Giza, kisha wakatoka. Walifanya nini? Jambo lile lile. Imekuwa ni siku ya . . . Haijaitwa mchana wala usiku. Walikuwa na mashirika ya kutosha, nao waliamini ya kwamba Yeye alikuwa Mwana wa Mungu, na wakatembea kwa nuru waliyokuwa nayo, wakaunda makanisa yao, wakajenga hospitali na shule na kadhalika, na seminari, na wakawapeleka watoto wao shuleni.

293 Lakini nabii alisema, "Itakuwa Nuru tena wakati wa jioni. Mwana atachungulia tena, itakuwa Nuru." Kitu gani? Mwana yeye yule (M-w-a-n-a) aliyefunuliwa katika mwili wakati wa asubuhi, huko nyuma, atafunuliwa tena wakati wa jioni.

294 Sasa linganisha Luka Mtakatifu 17:30, "Na katika siku hiyo, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, hali ya ulimwengu, katika wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa."

Itakuwa Nuru wakati wa jioni,
Njia ya kwenda Utukufuni hakika mtaipata.

295 Loo, jamani! Enyi watu, tuko wapi?

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara walizotabiri manabii;
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa na vitisho; (Uangalie ukizama baharini!)
Rudini, enyi mliotawanyika, makwenu.

Siku ya Ukombozi imekaribia,
Watu wakivunjika mioyo kwa hofu;
Jazweni na Roho, zitengenezeni taa zenu na kuzisafisha,
Angalieni juu! ukombozi wenu umekaribia. (Afadhali.)

296 Ndugu, dada, ni wakati wa kuogofya sana. Angalieni mambo yaliyotabiriwa, angalieni mambo hayo yakitukia. Angalieni unabii wote ukitimizwa, ndipo tuone haya yote yanahusu nini. Si kundi la. . .kipindi cha ushupavu wa dini. Ni Mungu akithibitisha Maneno Yake hasa, hasa. Mwamba umekwishapigwa, enyi marafiki, ukimbilieni upesi mwezavyo. Unabii unathibitisha siku tunayoishi.

297 Na tuinamishe vichwa vyetu. [Ndugu fulani ananena kwa lugha mpya. Dada fulani anafasiri. Ndugu fulani jukwaani anasema, "Je! tunaweza kutulia kwa muda kidogo tu? Mungu amenena nasi kupitia kwa Ndugu Branham, na upako uko juu ya Ndugu Branham, naye hajamaliza. Na . . . " Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

298 Mungu mpendwa! Je! mnatambua siku tunayoishi, marafiki? Ungethubutu kushindana na Mungu? Ungesema ya kwamba "Yeye amekosea," wakati amelithibitisha? Yeye Ndiye Anayejifasiria. Je! unataka kumtumikia?

Sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, na mioyo yenu imeinamishwa, ndugu, dada.

299 Huenda huu ukawa ndio wakati wetu wa mwisho wa kukutana. Huenda kamwe tusininii. . .Kama ningerudi mwaka mmoja tangu leo, kama nikiishi, kungekuwako na wengi walio hapa sasa hawatakuwa hapa wakati huo. Nami itanibidi kukutana nanyi kwenye Kiti cha Hukumu na kuwajibika kwa kila kitu nilichosema usiku wa leo.

300 Mbele za Mungu, wakati ukiwa na akili zako timamu, je! unaweza kumfanyia Mungu jambo hili? Kama unajua ya kwamba unaninii. . .Jingalie tu mwenyewe kwenye kioo cha kujiangalia cha Mungu (Biblia), haidhuru wewe ni nani, na useme, "Ninajua niko mbali sana na kuwa binti wa Mungu, angalia jinsi ninavyofanya. Niko mbali sana na kuwa mwana wa Mungu, angalia jinsi ninavyofanya. Lakini, Mungu, sitaki

kuwa hapa, ni—ninataka kujitahidi nipafikie mahali hapo." Ninakutaka umwinulie Mungu mkono wako, hata uwe u nani, popote ulipo kote jengoni, "Naam, ninataka kuwa mwana wa Mungu. Ninataka kuwa binti wa Mungu. Ninataka kutimiza kila kitu ambacho Bwana wangu ameamuru." Sasa wewe . . . Mungu akubariki. Ninakisia ni asilimia tisini ya wasikilizaji.

301 Sasa angalia hapa, rafiki yangu. Vipi kama ungaliishi katika siku ulizomsikia Yohana akihubiri? Vipi kama ungaliishi katika siku ambazo Yesu alikuwa hapa? Ungalichukua upande wa nani? Kama ungaliishi katika ninii za Yesu . . . Kumbuka, kama Yeye . . . Kama ungaliishi kule nyuma, ingalikuwa tu kama ilivyo sasa. Yesu yeye yule anajitambulisha kwa Neno Lake, unaona, na linachukiwa sana.

302 Lakini hebu nikwambie, mimi sijaribu kuwaambia watu waondoke kanisani ama . . . Jamani, ninawataka mwende kanisani, "Msiache kukusanyika pamoja." Lakini kile ninachojaribu kuwaambia mfanye ni mfanye bidii mwingie katika Ufalme wa Mungu. Mninii mambo haya, ulimwengu, kanisa . . .

303 Enyi Wapentekoste, ninyi watu mnakuwa wa kilimwengu sana. Mnaufuatilia sana ulimwengu. Ni rahisi tu, mnaendelea kuangalia televisheni na mambo haya yote, na jinsi wanavyofanya, na yote *haya*, na jambo la kwanza unajua . . . Seminari, shule zimeanza kupatana hapa na pale, na *hili*, *lile*, na *linginelo*, na muda si muda unajua . . . Halina budi kutukia hivyo. Kanisa la Kipentekoste, limekuwa msaidizi wangu mkubwa zaidi, siwezi kusema kitu dhidi yake. Lakini hiyo ndiyo sababu ninapaza sauti, "Ndugu zangu, tokeni!" Iteni . . . Hamna mikutano mliyozoea kuwa nayo. Watu hawako jinsi walivyokuwa. Lakini Yesu Kristo ni yeye yule, hebu tuingie ndani Yake.

304 Sasa, ninyi mlioinua mikono yenu, kumbukeni, kulikuwa na Mwamba uliopigwa nyikani, na chemichemi hiyo ingali imefunguliwa usiku wa leo. Mwamba wao umepigwa, Kristo, Yeye ndiye ule Mwamba uliopigwa.

305 Na usiku wa leo, nijuavyo mimi, huenda kanisa likaninii . . . Wakati wa kuitwa huenda umepita tayari, sijui, siwezi kusema jambo hilo. Kumbukeni, watu waliendelea moja kwa moja wakifanya mikutano, vivyo hivyo tu, baada ya kusulubishwa kwa Yesu. Na ninii . . . na watu wote, wata—watakuja, wataninii . . . Angalieni! Wa—wataendelea moja kwa moja kuhubiri, na wakisema "wanaokoka" na kila kitu, kama tu . . . "Ulimwengu unaendelea kama zamani," wanasema. Lakini kutakuwa kumechelewa sana wakati huo.

306 Wakati ukiwa na nafasi, ndugu yangu; wakati ukiwa na nafasi, dada yangu; njoo uingie katika Ufalme wa Mungu. Haikubidi kuingia chini ya kitu kingine chochote ila imani

rahisi ya kuamini Neno Lake. Yeye Ndiye hilo Neno! "Bwana Yesu, ninajua ninajiangalia mwenyewe sasa katika kioo cha Neno la Mungu; loo, jinsi nilivyopungukiwa. Lakini, Mungu mpenzi, hapa usiku wa leo, katika usiku huu wa Jumatatu, hapa San Bernardino, California, katika ukumbi huu hapa, haya—haya tu ndiyo yote niliyo nayo, Bwana, bali nitayatoa Kwako. Waweza kunichukua jinsi nilivyo, Bwana? Utanijalia kukimbilia msalabani upesi sana? Hata ninawaona wale wajumbe. Ninauona ule wakati, ninaona kule kuitwa kutoka Sodoma. Ninaona zile ishara. Ninaliona kundi la Ibrahimu likipokea ile Nuru. Ninaona dhihirisho, Yesu akidhihirishwa tena moja kwa moja miongoni mwetu kama ilivyokuwa. Ninaona mambo yote uliyoahidi. Ninaona waigaji; ninaona Wewe ulisema ya kwamba, 'Kama ilivyokuwa katika siku za Musa,' jinsi ambavyo huyu Yambre na Yane wangerudi wakaigize, na bado wabaki moja kwa moja kwenye lundo hilo la taka walilokuwa ndani yake."

307 Unaona, wasingeweza kumfuata Musa kupitia kwenye hilo Neno na kuwatoa watoto hao huko na kuwapeleka nyikani, kwa sababu walikuwa wamechangamana na Misri. Wasingeweza kufanya hivyo, ingawa walifanya kazi zile zile alizofanya. Lakini upumbavu wao ulidhihirika. Nayo Biblia inasema, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI, "Itatukia tena katika siku za mwisho."

308 Nanyi mnaona hayo kwa macho yenu wenyewe, kama ninyi ni wa kiroho. Ninaninii . . . Siwezi kuelezea jambo hilo. Haina haja mimi kulieleza. "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu." Hebu na tumwendee sasa, wakati tukiwa na nafasi. Sivyo?

309 Endapo unahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu, kama unataka kujiweka wakfu tena, maisha mapya; mchungaji wako hatakudharau, atakupenda kwa ajili ya jambo hilo. Jitoe kabisa kwa Mungu usiku wa leo, wakati tukiwa hapa. Hebu . . . Naam, ninajua umekuwa ni mgumu, wenye kukata, wa kipekee, sifanyi hivyo niwe mpinzani, ninafanya hivyo nipate kuwa mwaminifu. Ninafanya hivyo kwa sababu ninawapenda, ninampenda Mungu, na ninafanya hivyo kujaribu kuwasaidia. Na kwa kweli, ewe rafiki, ni—ni—ninaamini . . . Na kwa moyo wangu wote, kwa imani yangu yote, ninaamini ya kwamba Ujumbe wangu unatoka kwa Mungu. U—umekuwa ukiwathibitishia jambo hilo, miaka yote.

310 Sasa sikilizeni, usiku wa leo salimisha kila kitu ulicho nacho, kila kitu unachohitaji. Ninaamini, kwa moyo wa kweli, uliojisalimisha, kama utasimama tu kwa miguu yako, na kumwinulia Mungu mikono yako, na kusema, "Mungu mpendwa, mimi hapa. Nichukue, Bwana. Sitajaribu tena kutumia akili yangu mwenyewe na fasiri yangu mwenyewe. Neno Lako linasema sina budi kuwa 'mtakatifu, sina budi kuzaliwa mara ya pili, sina budi kujazwa na Roho, na ndipo Roho ataniongoza aniingize katika Kweli yote.' Mungu mpendwa,

mimi hapa, niongoze." Ungeweza kufanya kiasi hicho? Ukifanya hivyo, inua mkono wako, useme, "Niko tayari kufanya hivyo, niko tayari."

311 Basi hebu sote tusimame kwa miguu yetu.

> Nitwae hivi nilivyo,
> Umemwaga damu Yako,
> Nawe ulivyoniita,
> Bwana Yesu, (Mlango wa Mungu wa pekee) . . .
> naja! na . . .

Sasa chukua kazi yako yote, chochote kile, uchovu wako, kila kitu . . . Vipi kama ulikuwa ukifa sasa?

> Hivi nilivyo; si langu
> Kujiosha roho yangu;
> Nisamehe . . .

Hivi unaweza kuinua mkono wako juu, kwenye ubeti huu sasa?

> Naahidi, nitaamini
> Bwana Yesu naja! naja!

312 Sasa wakati mpiga kinanda akiendelea—anapoendelea kucheza, hebu kila mmoja wetu . . .

313 Enyi matineja vijana, mnataka kuwa kama hawa hapa nje mtaani, kundi hili la majambazi?

314 Dada, unataka kuwa na nywele fupi, wakati ni heshima yako ya Kinazarayo kwa Mungu kuwa na nywele ndefu? "Ni aibu kwake kukata nywele zake." Ungevaa maskini sketi hizi ndogo chafu na kadhalika wanazovaa siku hizi, nguo hizi—hizi chafu, zinazoonyesha mwili wako, huko nje mtaani? Je! ulijua kila mwanamume anayekuangalia anafanya uzinzi na wewe moyoni mwake? Nawe unajianika namna hiyo. Je! mnajua, enyi wanawake, ninyi mnaojipodoa, kuna mwanamke mmoja tu katika Biblia aliyepata kujipodoa? Naye Mungu akamlisha kwa mbwa. Yezebeli, jina ambalo limechukiwa tangu siku zake, kwa sababu ya matendo yake hayo. Mnajua nabii Eliya ndiye aliyelaani hayo na kumwita namna hiyo? Mnajua Herodia ndiye aliyefuatiliwa na Yohana Mbatizaji? Mnaninii . . . Hutaki kuwa kitu hicho cha Hollywood ya ulimwengu. "Ukiipenda dunia au mambo yaliyo katika dunia, kumpenda Mungu hakumo ndani yako."

315 Ndugu, rafiki mhudumu, hakuna kitu . . . Naomba unielewe, mimi ni ndugu yako. Je! unataka kujihusisha, na ninyi wafuasi wa kanisa fulani (Methodisti, Baptisti, ama chochote ambacho mmekuwa), je! unataka kushikilia dhehebu hilo kwa sababu mama yako na bibi yako walilishikilia? Yeye alitoka kwenye kitu fulani apate kuingia humo, hiyo ilikuwa ndiyo Nuru ya siku hiyo; hiyo, kama vile katika siku za Nuhu. Hii ni siku nyingine.

316 Unasema, "Vema, nilikuwa na ninii . . . "

317 Hii siyo siku ya Pentekoste. Wakati wa Pentekoste umepita. Pentekoste imekwisha, huu ni wakati wa mavuno. Unaona? Na wakati wa mavuno, ile punje; maji yamekwisha kumiminwa, punje inaiva. Ingia kwenye punje, ndugu yangu mpendwa. Nisikilizeni, niaminini, kama mnaniamini kuwa mtumishi wa Mungu, hebu kila mmoja, kwa njia yetu wenyewe, tuinamishe vichwa vyetu katika unyenyekevu na kuomba dua ambayo sisi—ambayo tunajua tunapaswa kuomba, "Mungu, nichukue jinsi nilivyo."

318 Nawe ndugu, dada, ninajilaza madhabahuni usiku wa leo, pia: Mungu, nifinyange na unifanye tofauti. Fanya jambo fulani, Mungu, nifanye katika mfano Wako.

319 Mnafikiri ni rahisi kusimama hapa na kuwakata watu vipande-vipande namna hiyo? Ni jambo gumu kufanya. Lakini ole wangu nisipofanya hivyo.

320 Mungu mpendwa, wakati wasikilizaji hawa wanapoinamisha kichwa chao na moyo wao, katika nyakati hizi zenye uchaji hapa za kumalizia hotuba hii ya Biblia; tunapoona thibitisho la Roho Mtakatifu ambalo lililitikisa taifa hili huku na huko, na huku na huko, ufufuo mkuu na dalili, tukijua ya kwamba kitu fulani kinapaswa kufuata jambo hilo. Halafu kuona hao Malaika saba wakishuka pale juu ya mlima ule huko Arizona, wakati hata magazeti kote nchini yalitangaza jambo Hilo. Kumwona Yesu Mwenyewe kule mbinguni, akiangalia chini, na kusema ya kwamba, "Katika Ufunuo 10:7, katika Ujumbe wa malaika wa saba, mihuri hii ingefunguliwa, siri za Mungu zingejulikana." Kwamba wale watengenezaji hawakuishi muda mrefu vya kutosha ku—kuielezea. Na hapa, hii mihuri saba iliyotia muhuri kitu hicho chote itafunguliwa katika siku hii. Kuona ishara hizi zote kubwa na maajabu ambayo yamefanywa, yamethibitishwa, yametabiriwa kabla hayajatukia, wala hakuna hata wakati mmoja umepata kutuacha, bali ulilitimiza kama tu vile lilivyosemwa.

321 Mungu mpendwa, tunatambua ya kwamba Yesu Kristo yuko miongoni mwetu. Tunajua ya kwamba Yeye yupo hapa. Yupo hapa usiku wa leo, Mungu asiyeonekana yupo hapa pamoja nasi, Naye anaweza kuthibitisha kila ahadi aliyofanya katika Neno Lake. Jinsi ambavyo umesimama na kuwathibitishia, migongo ikiwa imeelekezwa kwingine, katika mwanzo halisi kabla waigaji hata hawajaingia kwenye ulingo, Bwana, ama kuingia mbi—mbi—mbioni, kama tusemavyo. Ulionyesha na kuthibitisha, ukatabiri na kusema yale ambayo yangetukia barabara, na tunaona yametukia jinsi hiyo. Na Baba, Mungu, tunajua haiwezekani kuwa ni mwanadamu, haina budi kuwa ni Mungu. Kwa hiyo tunajua ni Wewe hapa usiku wa leo. Tusamehe dhambi zetu.

322 Mungu mpenzi, umeponya magonjwa yetu, sasa tu—tusamehe dhambi zetu, Bwana, za kutokuwa namna ya Mkristo tunayepaswa kuwa, sio . . . Tukikiri kwamba sisi ni mwanamume au mwanamke wa Injili-yote, na hapa tunajikuta tukiporomoka kama kuku wa kimadhehebu. Tusaidie, Mungu mpenzi, tuchukue na ututikise kwa Roho Wako Mtakatifu. Na kukiwa na kitu chochote ndani yetu kisicho kama Wewe, kiondoe kwetu, Bwana. Na uipande miguu yetu juu ya Neno Takatifu la Mungu, na umjalie Roho Mtakatifu aingie na kuuchoma moto moyo wetu na kuondoa takataka zote za kutokuamini na usingizi wa siku hizi; loo, tuinuke na kujitikisa. Tujalie, Mungu. Tusafishe! Tufinyange! Tuumbe! Mungu, tujalie hayo.

323 Kama kuna yeyote humu ndani usiku wa leo, Bwana, anayeshikilia moyoni mwake hiyo punje, ile jeni hai ya Mungu iliyokusudiwa Uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu; ninajua, Bwana, ya kwamba wamekusudiwa kusikia kwenye saa hii. Kwa hiyo, ninaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utaijaza nafsi yao na kuwaangazia ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu, na kuwatuma waende zao, wakifurahi na kushangilia.

324 Bwana Mungu, wao . . . Ninawakabidhi Kwako. Sijui hao ni akina nani, Wewe unajua. Mimi ninahusika tu katika kulihubiri Neno Lako, Bwana, unavyolifunua. Wewe unahusika na hayo mengine: mahali Mbegu inapoanguka. Mimi ninaitupa tu. Bwana Mungu, ninaomba ya kwamba ilianguka katika udongo mzuri, wenye rotuba usiku wa leo. Kusudi wengi walione, Bwana, na wainuke wakiwa Wakristo wanaonawiri katika siku hizi za mwisho, kusudi lile jambo kuu tunalotarajia lije, litakuja upesi. Tujalie, Bwana. Nawe utalichukua Kanisa Lako, Bibi-arusi Wako, na umpeleke nyumbani. Tunaona yote yamewekwa katika utaratibu. Njoo, Bwana Yesu. Tunayakabidhi yote Kwako, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya matokeo. Amina.

> Nampenda, Nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini . . .

325 Je! mnampenda? Vema, basi inawapasa kupendana. Peaneni mkono mnapouimba tena:

> Nampenda, Nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini . . .

326 Sasa hebu na tumpe *Yeye* sifa. Ni wangapi wanaoujua wimbo huu:

> Nitamsifu, nitamsifu,
> Nitamsifu Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
> ajili ya wenye dhambi;

Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

327 Na tuuimbe sasa:

Nitamsifu, nitamsifu,
Nitamsifu Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

328 Hivi hamsikii mmesuguliwa kabisa? Inueni mikono yenu na kusema, “Loo, hilo linanifanya kujisikia vizuri.” Ndugu, ninapenda hizo nyimbo za kale. Nanyi je? Zinaingia ndani moyoni.

Nitamsifu, nitamsifu,
Nitamsifu Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

329 Hebu na tuinue tu mikono yetu sasa na kumsifu Mungu, kila mmoja wetu, kwa njia yetu wenyewe:

330 Bwana Yesu, tunakushukuru. Tunakusifu, Bwana. Tunakutukuza kwa ajili ya watu walioitwa watoke, kutoka Babeli. Tunakushukuru kwa ajili ya Damu ya Mwanao, Yesu Kristo. Tunakushukuru kwa sababu Yeye anatusafisha dakika hii. Tunaninii. . .Tunaomba msamaha wa makosa yetu, ujinga wetu, Bwana, kujikwaa kwetu gizani. Ee Mungu, jalia tusimame na kuangaza, na kutembea katika Nuru ya jioni, na tuwe tunda la Mti unaokua kwa Nuru za jioni. Tujalie, Mungu mpendwa. Tunajikabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo.

331 Sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, ninawapa wachungaji wanaoiunga mkono ibada hii.

*MATUKIO YA SASA YANADHIHIRISHWA NA UNABII* SWA65-1206
(Modern Events Are Made Clear By Prophecy)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatatu jioni, tarehe 6 Desemba, 1965, kwa ajili ya dhifa ya Ushirika wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Ukumbi wa Orange Show huko San Bernardino, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2013 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org